# USHAWISHI

Habari za asubuhi, vizuri sana kuwa hapa asubuhi ya leo, kusikia taarifa hii nzuri ya jinsi kazi ya Bwana inavyopanuka. Hiyo ndiyo sababu ya sisi kuwa hapa. Hilo ndilo sikuzote tunafurahia kusikia, kupanuka kwa kazi ya Bwana.

2 Basi nilipoamka asubuhi ya leo, ni—nilidhani niliwafanyia uovu, ni—nilileta baadhi ya hali ya hewa ya Indiana huku kuwatembelea. Mimi, kwa—kwa mara yangu ya kwanza, niliona barafu Phoenix; nje ya nyumba ya barafu, mwajua. Lakini—lakini hii ilikuwa barabarani asubuhi ya leo, barafu. Mke wangu aliamka naye akasema, "Hii ni Phoenix?"

3 Nikasema, "Nafikiri ndiyo." Nikasema, "Sikufikiria tuliingia vibaya jana usiku." Lakini hakika ilikuwa inashangaza kuona barafu Phoenix. "Vema," nikasema, "kama unaweza tu kuzinduliwa vya kutosha kuja huku kwenye kiamshakinywa, barafu yote itayeyukia kule, maana Uwepo wa Bwana sikuzote huyeyusha ubaridi wote."

4 Furaha sana kuwa hapa asubuhi ya leo pamoja na Ndugu na Dada Williams, na Ndugu Rose, na wahudumu wote. Pia furaha sana kurudi kwenye Ramada tena. Kuna kitu fulani kuhusu mahali hapa. Ninapaona wakati nikisafiri barabarani, ninawazia kuhusu mikutano nimekuwa nayo humu, awali, ya Ramada. Nasi tupo hapa sasa kuanzisha mfululizo wa mikutano pamoja na ndugu zetu wa huku kote bondeni, kabla ya m—mkutano mkuu wa wafanyabiashara.

5 Basi ni wahudumu wangapi walio hapa asubuhi ya leo? Hebu tuione mikono yenu, kila mahali. Loo, hii ni . . . Vema, tuko katika shughuli basi. Tungali tunawajulisha kwamba sisi tuko katika shughuli, pia, shughuli iliyo kuu sana ulimwenguni, kuokoa nafsi. Nasi wahudumu bila shaka tuna furaha asubuhi ya leo kushikana mikono na watumishi hawa wa—walei Wakristo, pia, kwa wasaidizi na wenzi katika kazi hii, kusaidia kuwaokoa watu kwa Ufalme wa Mungu. Tunashukuru sana kwa jitihada hii!

6 Nilikuwa nikisikiliza hivi majuzi kwenye matangazo ya redio, nilipokuwa nikiendesha gari, na kulikuwako na hakimu aliyetoa ta—tamshi ambalo nilidhani lilikuwa ni zuri sana. Akasema, "Ni kwa nini, kwamba, katika siku hizi, ambapo tunajua kwamba tunakabili wakati wa mwisho," akasema, "na kuona walei na wahudumu wanaketi tu kitako wala hawaichochei hasira yao ya haki, kuona ulimwengu umezama sana katika dhambi jinsi ulivyo, ambapo wahudumu na walei pia wanapaswa kufanya bidii kila wakati, kwa kule Kuja kwa Bwana, kunakokaribia sana. Nasi hutuonekani

kuchangamshwa sana kukuhusu, jinsi tunavyopaswa kuwa." Nilikuwa nikizungumza hivi majuzi juu ya somo la kuwa waaminifu.

7 Sasa, tunaamini, kama watu wa full Gospel, kwamba tunayo ile Kweli, ile Kweli ya Injili. Tunatambua kwamba kuna mengi tunayoweza kuboresha, juu ya hii.

8 Nasi tunautazamia wakati ambapo . . . sehemu zote legevu za miamsho hii mikubwa ambao umepitia kote ulimwenguni katika karne chache zilizopita, vema, tangu kule kuanguka kwa kanisa, na halafu ule wakati wa giza. Ndipo hawa mashujaa wakuu wakatokea, kwa ajili ya ile Kweli, nao wangeishi muda mrefu kutosha kwa namna fulani kuutambulisha nusu, kisha sehemu legevu zingeisha.

9 Tunaambiwa, katika Ufunuo 10, ya kwamba kutakuwako na mjumbe katika siku za mwisho, atakayekusanya maskini sehemu hizi na kuzileta pamoja. Ndipo siri ya Mungu itakapotimizwa, katika kutoa sauti kwa malaika huyu, ambaye alikuwa ni mjumbe wa duniani. Ndipo mmoja akashuka kutoka Mbinguni, ameinua mikono Yake, upinde wa mvua juu ya kichwa Chake, na kuapa kwamba hakutakuwako na wakati baada ya haya; Malaika akila kiapo. Basi tunapoona kitu hiki kikitokea, loo, jinsi tunavyopaswa kuwa waaminifu.

10 Ahadi zote za Mungu ni za kweli, bali zina masharti. Haijalishi tuko sahihi vipi kimsingi, hatuna budi kulikaribia kwa njia nzuri. Sasa, watu wanaweza kuwa sahihi kimsingi, na bado wasizipokee baraka za Mungu kwa sababu zimeendewa kwa njia mbaya. Zinaenda kwa masharti.

11 Kwa mfano, wakati Ahabu na Yehoshafati walipokuwa pamoja. Nayo Ramothi-giliadi kweli ilikuwa ni mali ya Israeli, kimsingi, kwa sababu nchi hiyo iligawanywa na Yoshua, kupitia kwa Yoshua, na Mungu, ilikuwa imepewa Israeli. Nao Washamu walikuwa wakiichukua hi—hiyo nchi na kuyajaza matumbo ya adui, kwa chakula ambacho kilipaswa kupewa Israeli. Kimsingi, Ahabu alikuwa sahihi. Na hiyo ndiyo sababu manabii mia nne wa Kiebrania, kwa moyo mmoja, walikuwa wakitabiri, "Kwea Ramothi-giliadi." Kimsingi, walikuwa sahihi. Lakini Ahabu hakuwa sahihi, yeye mwenyewe.

12 Basi wakati maskini mtu huyu mmoja aliposimama, jina lake Mikaya, mwana wa Imla, na kuona ono. Sasa, ono la mtu mmoja, dhidi ya manabii mia nne waliofunzwa, bali ono la mtu huyo lililingana na Neno. Hiyo ndiyo sababu yeye alijua lilikuwa ni la kweli. Na, mnaona, ni kwa masharti. Hatuna budi kuwa na hakika.

13 Wakati Hanania alipotabiri, na kuitwaa nira kutoka shingoni mwa Yeremia.

14 Kwamba, Israeli walikuwa wawe vyombo vya Bwana, hasa, huko chini na chini ya Nebkadreza, nazo falme zote

jirani zilikuwa zimetolewa kwa kafiri huyu Nebkadreza huko chini katika Babeli. Hawa hapa Israeli wakitoa dhabihu zao, na wa kidini na kimsingi tu walivyoweza kuwa, bali hata hivyo ule uaminifu ulikuwa umeondoka. Nao walitolewa huko chini kama—kama watumwa wa kumtumikia Nebkadre-. . . Nebkadreza kwa miaka hii yote. Basi Yeremia alikuwa na nira shingoni mwake. Naye Mungu alikuwa amemwambia, "Haijalishi ni nabii yupi anayetabiri, ni mwotaji yupi anayeota, ama chochote kinyume na yale Yeye aliyosema, ilikuwa ni makosa."

15 Naye huyo hapo Hanania amesimama. Hanania, mwaminifu tu kama mtu yeyote angaliweza kuwa, naye akatabiri kwa ujumbe, "BWANA ASEMA HIVI." Vema, hakika hao watu wangeweza kupiga makofi juu ya hilo. Hiyo ni kweli. "BWANA ASEMA HIVI. Wao, yeye ataninii, watarudi katika miaka miwili, katika muda wa miaka miwili kamili." Ndipo akamwendea nabii huyo aliyethibitishwa, akaitwaa hiyo shingoni mwake akaivunja. Akasema, "BWANA ASEMA HIVI."

16 Mnakumbuka yale Yeremia aliyosema? "Hanania, amina. Na iwe hivyo. Bwana ayatimize maneno yako. Lakini hebu na tukumbuke, kumekuwako na manabii waliotutangulia. Walitabiri dhidi ya falme mashuhuri, dhidi ya vita, kadhalika. Lakini nabii anajulikana tu wakati unabii wake unapotimia." Basi Hanania akaivunja ile nira. Basi mnajua yale Mungu aliyomwambia.

17 Nafikiri sisi watu wa Kipentekoste. . .Kimsingi, full Gospel ni Kweli, bali kuna mengi yanayoambatana nayo: ni ule uaminifu wenye kilindi wa kile Mungu ametupa, hatuna budi kukikaribia kwa heshima, na—na upendo, na katika mtazamo mnyenyekevu. Nafikiri hilo ndilo tunalohitaji.

18 Na sasa, katika mikutano hii ijayo, si—sijui hasa mahali ninapoenda, Ndugu Williams. Ni kote kutoka mahali hadi mahali, miongoni mwa ndugu zangu. Ninyi nyote ombeni ya kwamba Mungu atatusaidia, kwamba kutakuwako na wagonjwa watakaoponywa. Na kutakuwako. . .Jambo la kwanza, hebu niseme, kwanza, kutakuwako na nafsi zitakazookolewa, na—na waaminio kujazwa na Roho Mtakatifu, wagonjwa kuponywa, Mungu apokee utukufu, nalo Kanisa Lake likue kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

19 Nami nipo hapa kusaidia kwa kila njia niwezayo. Katika hili, ninao, nafikiri, sana sana ni watu wa full Gospel, A—Assemblies of God, na Foursquare, na church of God, na ndugu wa Umoja, na wote—wote pamoja. Basi hivyo ndivyo ni—nipendavyo, ambapo tunaweza kwenda kila mahali, na wote wakusanyike pamoja.

20 Pentekoste kwa kweli si dhehebu. Ni tukio. Kwamba, tunapata kwamba maskini mawazo yetu yalivyokuwa, katika miaka iliyopita, kwamba, "Kundi moja tu, lililoitwa

Wapentekoste, ndilo tu lililopata baraka hii." Tunaona ya kwamba Mungu aliyararua tu maskini mawazo yetu vipande-vipande. Akawaingiza Wakatoliki, Presbiteri, Wamethodisti, Wabaptisti.

21 Akawapa Roho Mtakatifu hao wanaomtumikia, waliofanya mapenzi Yake, na Yeye habadiliki. Hawezi kubadilika. Msimamo Wake hauna budi kuwa ni ule ule sikuzote. Maamuzi Yake ni makamilifu, kwa kuanzia. Haimbidi kubadilisha chochote, Maneno Yake. Yeye ni mwenye enzi. Haimbidi kubadilisha chochote, na Yeye habadiliki.

22 Kwa hiyo tuna furaha asubuhi ya leo ya kwamba Kristo yu hai. Na kama vile wimbo usemavyo, "Mnajuaje Yeye yu hai? Anaishi mioyoni mwetu." Nasi tunajua hilo. Tuna hakika na jambo hilo.

23 Kwa hiyo tukiukaribia uamsho, ujao, kutoka kanisa hadi kanisa, halafu kurudi hapa Ramada kwa ajili ya ule mkutano mkuu, hebu twende kwa uchaji, uaminifu wenye kilindi, wanyenyekevu, tukiomba, na kumwamini Mungu.

24 Sasa, ninajua sisi hukaa muda mrefu kidogo, kila wakati, bali sitaki kufanya hivyo katika mikutano hii. Ninataka kuingia mle, na kuwaacha watu watoke, niende nyumbani, na nifanye yale niwezayo kwa ajili ya Ufalme. Na niende mahali fulani, na kuomba usiku kucha, kama nikitaka kuzungumza kidogo na Bwana, wala nisiwacheleweshe wakati nikifanya hivyo.

25 Na sasa, asubuhi ya leo, ninajisikia kana kwamba kiamshakinywa hiki kidogo ni mlango wa. . .Huu ni alfa, na hatimaye mkutano mkuu ni omega ya—ya huu uamsho.

26 Na sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kidogo tu, kwa uaminifu, tunapokikaribia kiti Chake cha rehema. Na hapana shaka ila kwamba kuna haja nyingi hapa ndani asubuhi ya leo. Lakini wakati tukiomba, nawe ungetaka kukumbukwa, unaweza kuinua tu mkono wako, nawe ushikilie chini ya huo ile siri unayomtaka Mungu akutendee. Asanteni.

27 Mungu aliye mtakatifu sana na mwenye uchaji, Mwenyezi, tunakikaribia Kiti Chako cha Enzi sasa, tunapokuja kutoka mahali hapa panapoitwa Hoteli ya Ramada. Kwa imani, tunapita zaidi, ya mwezi, nyota, juu ya kundi jeupe la nyota, hata kuingia katika Uwepo wa Mungu, tunaposimama karibu na Kiti Chake Cheupe cha Enzi, tukiangalia ng'ambo kwenye zile Nuru za dhahabu ambako Mungu pekee ndiye anayeweza kuishi. Tunaona, kati ya sisi na madhabahu haya, kunayo Dhabihu yenye Damu iliyowekwa Pale. Kama vile ndugu yetu na dada walivyolielezea, muda mfupi uliopita, "Yule aitwaye Yesu." Naye aliahidi, alipokuwa hapa duniani, "Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, nitalijalia." Hapo tunamwona leo hii, amesimama hapo kutimiza kila Neno na kila ahadi aliyotoa.

28 Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, kwamba Wewe utaturuhusu kuingia katika Uwepo Wako, kwa uaminifu, na kwa imani, tukiamini sasa ya kwamba Wewe utajibu hili tuombalo. Na la kwanza kati ya mambo yote, tunajiombea wenyewe, msamaha wa makosa yetu yote, na mambo yote tuliyofanya, ambayo yangekuwa ni yasiyohesabika, Bwana. Nasi tunaomba ya kwamba Wewe utatusamehe, na ujalie hiyo Damu ya thamani ya Dhabihu madhabahuni, asubuhi ya leo, itusafishe na maovu yote, uchoyo wote, na yote yaliyo kinyume, Bwana, na amri Zako kuu na mapenzi Yako kwetu.

29 Tujalie sisi, asubuhi ya leo, Bwana, katika njia nyingine, ama wakati mwingine, tujiweke wakfu Kwako, na katika unyenyekevu wetu tuamini ya kwamba Wewe utauchochea uamsho kupitia kwenye bonde hili. Nasi tu wanyonge sana, Bwana. Kujaribu kudiriki jitihada kuu namna hiyo, isingewezekana kabisa. Lakini Wewe, Ee Mungu, unaweza kuchukua vitu vilivyo dhaifu vya duniani na unaweza kufanya kazi kuu za Mungu kwavyo. Tunajinyenyekeza kama waaminio, na kuomba ya kwamba Wewe utavichukua vyombo hivi dhaifu, nawe utatenda kazi Zako kupitia kwao, tupate kuona matokeo makuu hapo mkutano huu utakapokwisha, kwamba kazi ya Mungu imeanza kudhihirishwa upya katika bonde hili.

30 Wabariki ndugu zetu wote, makanisa, kila dhehebu, wafuasi wake wote. Nao wafanyabiashara hawa, walei hawa ambao wameyaweka wakfu maisha yao Kwako, tunaomba, Baba Mungu, ya kwamba Wewe utawabariki katika mkutano wao ujao. Kwa jumla, Bwana, fanya utukufu Wako kupitia kwetu, ili wengine waweze kuona mambo mazuri ya Mungu, na wawe na shauku ya kumtumikia. Tunayakabidhi mambo haya Kwako pamoja na upendo na heshima, na imani, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

31 Sasa ningependa, asubuhi ya leo, Mungu akipenda, kuyafungua Maandiko, mkitaka sasa, kwenye kitabu cha Isaya. Na huu ukiwa ni mkutano wa wafanyabiashara, hata hivyo shughuli yao kuu ni kuwafanya watu kujiweka sawa na Mungu. Hilo ndilo wamejitolea kufanya kwa dhati. Nasi tunataka kuzungumza juu ya Injili, na uaminifu na njia ya kuiendea. Na hebu tuanze kusoma sasa kutoka katika Isaya 6, mla- wa kwanza. . .Ama kifungu cha kwanza cha Isaya 6, tuendelee kusoma, pamoja na cha 8.

> Na *katika mwaka ule aliokufa mfalme Uzia nalimwona Bwana ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu. . ., kimeinuliwa sana, na pindo za vazi lake zikalijaza hekalu.*
>
> Na *juu yake walisimama maserafi; kila mmoja. . . alikuwa na mabawa sita; kwa mawili alifunika uso*

*wake, na kwa mawili alifunika miguu yake, na kwa mawili aliruka.*

*Wakaitana, kila mmoja* na *mwenzake,. . .kasema, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni Bwana* Mungu *wa majeshi: dunia nzima imejaa utukufu wake.*

*Na misingi ya* milango *ikatikisika kwa sababu ya sauti yake aliyelia, nayo nyumba ikajaa moshi.*

*Ndipo niliposema, Ole wangu! kwa maana nimepotea; kwa sababu* mimi ni *mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu: na macho yangu yamemwona Mfalme, Bwana wa majeshi.*

*Kisha mmoja wa maserafi wale akaruka akanikaribia, naye alikuwa na kaa la moto mkononi mwake, ambalo alikuwa amelitwaa kwa makoleo toka juu ya madhabahu:*

*Akanigusa kinywa changu kwa kaa hilo, akaniambia, Tazama, hili limekugusa midomo yako; na uovu wako umeondolewa, na dhambi yako imefunikwa.*

*Kisha nikasikia sauti ya Bwana, akisema, Nimtume* nani, *naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa; nitume mimi.*

32 Ninataka kutoa kutoka kwenye fungu hili dogo, muktadha fulani, juu ya muhtasari fulani ambao nimeandika hapa. Na kama ningeupa anwani, ningetaka kuuita: *Ushawishi.*

33 Mnajua, kuna wengi sana wetu, na karibu sisi wote humshawishi mtu fulani kwa mambo tufanyayo, na jinsi tunavyoishi, na mambo tusemayo. Tunamshawishi mtu fulani. Mtu fulani anayaangalia maisha yako. Na basi wakati tunapokiri kuwa Wakristo, inatupasa kuishi maisha ya jinsi gani ikiwa mtu fulani anatuangalia? Nayo maisha yako unayoishi yataakisi ushawishi juu ya mtu fulani. Hiyo huenda. . . Huenda ikawa. . .Kikomo chao cha Milele kitatulia juu ya jinsi unavyoishi na mambo ufanyayo, kwa kuwa wanakuangalia.

34 Katika somo letu asubuhi ya leo, kama *Ushawishi,* tunaona ya kwamba huyu Mfalme Uzia alikuwa u—u—ushawishi mkubwa juu ya Isaya, na—nabii kijana. Isaya alikuwa ameitwa karibu naye, akiwa ni nabii wa siku hizo aliyejulikana, aliyethibitishwa. Naye alikuwa na. . .Ninaamini jinsi Isaya alivyolinena, alikuwa ninii—ninii. . .alikuwa na ushawishi mkubwa juu ya Isaya.

35 Sasa, tunaona ya kwamba Uzia aliitwa kuwa mfalme kwenye umri wa yapata miaka kumi na sita, baada ya kifo cha baba yake. Naye baba yake alikuwa mwa—mwaminio mashuhuri. Naye alikuwa. . .Mama yake pia alikuwa ni mwanamke mzuri sana. Basi mfalme huyu kijana alikuwa amevikwa taji kwenye umri wa ujana, na upesi akachukua njia iliyokuwa sahihi, kwa sababu ya ushawishi wa baba mtauwa na mama mtauwa.

36 Nami nafikiri huo ni mfano mzuri sana kwetu wazazi siku hizi, ni kuweka mfano mbele ya watoto wetu. Sasa, utaishi maisha ya—yako yaliyo bora zaidi na yaliyo mabaya zaidi nyumbani. Nami nafikiri kwamba maisha yetu . . . Ingawa huenda watoto kabisa wasitende tu kana kwamba wanayaona, bali wanayaona. Kamwe usiwazie kwamba hawayaoni, kwa sababu wanaangalia.

37 Sio tu watoto wanaangalia, bali majirani wanaangalia. Sio tu majirani wanaangalia, bali nanii . . . wote ambao unashirikiana nao, wanakuangalia. Watu kanisani mwako wanakuangalia. Watu unaofanya bishara nao sokoni, wanakuangalia, baada ya maungamo yako. Nasi inatupasa sikuzote kujaribu kumwakisi Kristo katika kila kitu tufanyacho.

38 Ninajua msemo mdogo ambao niliutundika nyumbani mwangu miaka mingi iliyopita. Niliuchukua wakati mmoja nilipokuwa kwenye maskani ya Billy Sunday, nilipokuwa kwenye mmoja wa mikutano hiyo huko kwenye—kwenye Ziwa Winona. Nami niliupenda sana hata ni—nikauchukua. Nikautundika nyumbani mwangu, nami nikauweka mpaka ukararuka tu. Ulikuwa kitu kama hiki. "Usiende mahali popote ambapo usingetaka kupatikana kama Yesu angekuja." Na, "Usiwe ukisema chochote ambacho usingetaka kuwa ukisema kama Yesu angekuja." Nao ukaendelea pamoja na mambo mengi, ukisema yale wewe . . . Vinginevyo, lolote ufanyalo ama kusema, ama tendo lolote unalofanya, usilitende iwapo usingetaka kukutwa katika hali hiyo Yesu ajapo. Laiti tungalifanya tu hivyo, nina hakika tungekuwa ushawishi mkubwa juu ya wenzetu. Nanyi mnajua yaliyo mema. Kunazo njia mbili za kufanya lolote, hizo ni iliyo sahihi na isiyo sahihi.

39 Nilikuwa na maskini mwanangu, Joseph, pajani mwangu, hivi majuzi. Nami nikamwambia . . . Yeye ana umri wa miaka minane. Basi mvulana fulani mdogo alikuwa amemchokoza, ndipo yeye na mvulana huyo mdogo wakapigana. Kwa hiyo nikasema, "Joseph, usifanye, usifanye hivyo."

Akasema, "Lakini, baba, yeye alinifanyia *hivi na vile*."

40 Nikasema, "Lakini hilo halijalishi, unaona, yale aliyofanya. Kumbuka tu, Joseph, hilo. Unampenda baba yako?"

Akasema, "Naam, baba."

41 Nikasema, "Basi kumbuka, kwamba watu watayaangalia maisha yako kama mwana wa mhudumu. Ndipo basi kama ukifanya lolote baya, basi watasema, 'Hivi mhudumu huyu anamruhusu mtoto wake kufanya hivyo?'"

42 Sasa, tunajua wao hufanya hivyo, haidhuru. Lakini tunajua hilo. Kama Wakristo, tunajua ya kwamba tunajaribu kuwalea watoto wetu vizuri. Lakini ni jambo jema kuweka hilo mbele—mbele yao wakati wote, kufanya yaliyo mema. Usininii, kamwe usiuchukue upande huo mwingine.

43 Kwa hiyo nikasema, "Kwa sababu, unaona, hilo halikuletei tu sifa mbaya, Joseph, bali linamletea mama yako sifa mbaya, linawaletea dada zako sifa mbaya. Linamletea baba yako na kusudi lote la familia, yale tunayotetea. Halafu yale tunayotetea, linaleta sifa mbaya kwake, kwa Yesu Kristo. Hutaki kufanya hivyo." Nikasema, "Bwana we—wetu alitwambia kama tukininii . . . mtu akitupiga shavu moja, geuza tu la pili."

44 Na, hakika, hilo kidogo ni gumu kwa mvulana mdogo mwenye hasira kali, kwanza kabisa, ku—kuwazia mambo kama hayo. Lakini yaweke mbele zake, kwa vyovyote vile, unaona, kwamba haimpasi kufanya hivyo.

45 Sasa, jamaa huyu mdogo, Uzia, alikuwa na mafunzo kama hayo katika siku zake za mwanzoni, mpaka, wakati alipokikalia kiti cha enzi, kamwe hakugeuka kulia wala kushoto, kutoka kwenye jambo lililokuwa jema. Yeye alidumu moja kwa moja nalo. Hakuacha siasa zimshawishi kwa njia yoyote. Yeye alikuwa ni mtu aliyedhamiria kumtumikia Mungu, kwa vyovyote vile. Na kwa hiyo siasa hazikuninii . . . Aliyapuuza mambo hayo yote. Na jambo lingine nililopenda kumhusu Uzia, ni kwamba alipuuza kupendwa sana na watu ama maoni ya watu wengi. Haijalishi mtu mwingine yeyote aliwaza nini, ama mtindo uliopendwa na wengi wa siku hizo ulivyokuwa, yeye alitaka kumtumikia Mungu, haidhuru.

46 Loo! Tunahitaji watu kama hao katika ulimwengu wetu wa siasa. Tunahitaji watu kama hao katika Ikulu. Tunajitaji watu kama hao katika biashara. Tunahitaji watu kama hao mimbarani, watu ambao hawatageukia maoni ya watu wengi ama kupendwa na watu, bali watakaa moja kwa moja pamoja na Neno, sio kugeuka kulia wala kushoto.

47 Mungu, katika kumwagiza Yoshua, alisema, "Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali ukitafakari mchana na usiku. Ndipo utakapozifanikisha njia zako. Ndipo utakapositawi sana."

48 Na si hilo tu, bali unamshawishi mtu fulani sawasawa na unavyosafiri.

49 Na kwa hiyo ninathamini msimamo huu ambao Uzia alichukua, kuyakinia. Jambo la kwanza aliloanza kufanya, lilikuwa ni kuitengeneza nyumba ya Bwana, na kujenga mahali ambapo palikuwa pamebomolewa. Kisha kwenda kwa adui, akiisha kumthibitishia Mungu kwamba alikuwa ni mwaminifu. Naye a—alikuwa achukue msimamo mzuri, bila kujali yale watu majirani wake, washauri wake kumshawishi kwa upande wa kisiasa wa—wa ufalme. Yeye asingevumilia hilo. Yeye alitaka mapenzi ya Mungu na hayo pekee.

50 Hao ndio aina ya wanaume tunaohitaji. Namna ya akina mama tunaohitaji, mwanamke, mama wa siku hizi, ambaye atachukua msimamo sahihi na kufanya yaliyo mema. Haijalishi

wanawake wengine wanafanya nini, wewe fanya yaliyo haki. Ni huzuni sana kuliona taifa letu katika njama liliyomo siku hizi.

51 Niliamka, kidogo nimechelewa asubuhi ya leo, kwenda kula kiamshakinywa. Nilienda mahali, kunywa kahawa kidogo. Basi maskini msichana mmoja akaja kunihudumia. Naye alikuwa . . . Mimi na mke wangu tulikuwa tumeketi pale. Naye alikuwa ameyapaka macho yake samawati, mwajua, kitu—kitu hicho juu ya macho yake.

52 Nami niliona mmoja wa hao huko Los Angeles wakati mmoja, wa kwanza niliyepata kumwona, kina mama walijipodoa jinsi hiyo. Ni—ni—niliwazia hilo. Ni—nilikuwa nimwendee nimwambie nilikuwa mmishenari, nami nilikuwa nimeona pelagra na ukoma, na, bali sikuwa nimewahi kuona kitu kama hicho. Nami nilitaka kumwomba kama nisingeweza kumwombea, na—na, sasa, naye aniambie ni ugonjwa wa namna gani aliokuwa nao. Nami kidogo niliogopa. Nami kamwe sikuwa nimeona kitu mfano wake. Nami, wakati nilipomwendea . . . Nilikuwa nikimngojea Ndugu Arganbright na mmoja wa wafanyabiashara, na hao maafisa. Ndipo msichana mwingine akatokea, alifanana naye kabisa. Nikawaza, "Aisee, hu—huenda nimekosea hapa. Huyo, huenda amejifanyia hivyo mwenyewe." Naye alikuwa ni msichana wa kuvutia sana, angalikuwa, laiti angalikuwa tu ameuosha uso wake na kuonekana kama mwanadamu. Lakini alikuwa ninii sana . . .

53 Sasa, wakati baadhi ya hawa mabingwa wa sinema, ama mahali fulani (sijui inatoka wapi), watakapofanya jambo kama hilo, mwanamke fulani aliye na ushawishi wa namna fulani, basi hilo linalishawishi taifa lote kujaribu kufanya vile vile. Hiyo ni kweli.

54 Wakati wanawake wetu wa Kipentekoste waliporuhusiwa kukata nywele zao, kwa sababu mhudumu fulani aliachilia mimbarani, basi hao wengine walisema, "Vema, mke wa *Nanii* hufanya hivyo. Na sisi je?" Mnaona, ni ushawishi unaoweka juu yake, baadhi yao.

55 Maskini msichana huyu asubuhi ya leo alikuwa ni msichana mzuri sana. Alikuwa mzuri sana, na mwenye heshima alivyoweza kuwa. Basi wakati sisi . . . Alipoondoka mezani, na kugeuka. Mke wangu aliniangalia upande wa pili wa meza. Ndipo nikasema, "Unajua, ni huzuni tu kwamba ibilisi fulani . . . " Nami sisiti kusema, "ibilisi." "Ambaye amebuni kitu kama hicho, kuwaleta wanawake wetu wa Marekani chini ya ushawishi kama huo wa tabia hizo za kikafiri." Ushawishi! Mtu fulani aliuanzisha.

56 Lakini kamwe usifuate yale, unaona, mtu fulani wa nchi hii, sijali, nchi nyingine, ama—ama mke wa mhudumu fulani, ama mtu mwingine. Kamwe usishawishiwe nao. Acha Biblia ikushawishie jambo lililo sahihi.

57 Na hilo ni kosa, sasa. Halafu basi tu—tunapaza sauti, na kucheza dansi, na kunena kwa lugha. Na—na utukufu wa Mungu, tunadai, uko juu yetu. Na halafu tuliendee jambo kama hilo? Kuna kasoro fulani.

58 Sasa, ninaamini katika mambo haya, huku kupaza sauti, na kunena kwa lugha, na kucheza katika Roho.

59 Lakini, ndugu, Mungu angewezaje kuvumilia kitu kama hicho, wakati Yeye anakipinga? Naye anasema hivyo katika Neno Lake. Nao wanawake wetu wamekuwa katika makanisa yetu, ambalo wanalifanya mara nyingi, kuvaa nguo, kuvutia kijinsia. Linanenwa kwa nadra sana mimbarani. Na hata hivyo tunapaza sauti, na kuruka-ruka, na kunena kwa lugha. Hiyo ndiyo sababu mwenendo huu mkubwa unaoitwa Pentekoste hauendi popote, ni kwa sababu hakuna uaminifu nyuma yake. Unakuwa ni mhemko.

60 Na kwa sababu kuwa mimi husema mambo hayo, wengi husema, "Yeye ni mchukia wanawake. Yeye, yeye ni tofauti na. . . "

61 Sio kujaribu kuwa tofauti. Ni kujaribu kuwa mwaminifu. Ninaamini kwamba tuko katika siku za mwisho. Nasi tunao Ujumbe mkuu, bali kupiga kwetu kwote makelele na kunena kwa lugha hakutakuwa na matokeo yoyote. Unaweza kuliona miongoni mwetu. Unaweza kuona kwamba idadi yetu inaongezeka, bali je, tunakua katika nguvu? Tungali mahali pale pale tulipokuwa tulipoanza miaka arobaini iliyopita. Ambapo, inatupasa kuwa katika nchi ya ahadi tayari.

62 Ushawishi! Mke wa mhudumu mmoja aliachilia na kufanya jambo *hili*, na mhudumu mmoja akaanza *hili-na-lile*, ndipo hao wengine wakaanza tu. Loo, sisi nasi, kama Uzia hapa, na—na tusiache chochote kitushawishi ila Neno la Mungu. Hebu Hilo liwe ndilo ushawishi wetu. Tujirejeshe kwenye ile Imani, turejee kwenye sahihisho la Maandiko, haijalishi yale ulimwengu wote ufanyayo.

63 Na sisi ndugu, wengi wa ndugu ambao ni wafuasi wa dhehebu, ambalo, kwa jumla, lote lina vikundi vidogo, sina neno dhidi ya hilo. Hilo ni sawa. Lakini wakati tunapofikia mahali ambapo tunajisikia, kwamba, "Letu ndilo kundi la pekee." Kwamba, "Tunalo. Jamaa huyo mwingine hana uhusiano wowote na Hilo." Hiyo ni kushawishiwa na wenye vyeo katika dhehebu hilo, kwamba, "Inatupasa kulikuza dhehebu letu." Inatupasa kuukuza ule Ufalme. Mnaona? Tupo hapa kushawishi. Wala kamwe hatutakuwa ushawishi kwa ulimwengu wa nje mradi tu tunajaribu kuwashawishi kwa dhehebu fulani, kwa sababu wamekuwa hivyo kabla hatujazaliwa. Hebu tumtetee Mungu na Neno Lake, na kufanya ushirika na tuwapate ndugu wote. Hebu na tusichore mstari na kusema, "Usipouzingatia *huu*." Hebu tunyoshe mkono kupita huo mstari, tuwe ndugu.

64 Hiyo ndiyo sababu nimeuzingatia sana Ushirika huu hapa wa Wafanyabiashara Wakristo wa Full Gospel. Hiyo ndiyo sababu kwamba Wamethodisti na Wapresbiteri na kadhalika, ambako wahudumu wasingeweza kuonekana kuifikia ng'ambo ya pili huko, bali Wafanyabiashara walivunjilia mbali mapokeo hayo. Wanasaidia, kufanya jambo hilo. Sasa, kama tunaweza tu kuliondosha vichwani mwao, kuunda dhehebu; ambalo, inaonekana kana kwamba wanaelekea huko. Basi watakapofanya hivyo, mimi siko, kwa sababu nipo hapa kutetea kile kilicho kweli. Mnaona? Mnaona? Mnaona? Kamwe hatutaki hilo. Jambo ndilo hilo, ninii tu . . . Ningetaka kuzungumzia, moja ya siku hizi usiku, "Samsoni, simama mahali papo hapo," kwa hiyo mahali fulani tunapoendelea. Sasa, hebu tuone ushawishi wetu ulicho.

65 Sasa tunaona, Uzia hapa, yeye alikuwa ni mtu mashuhuri. Nasi tunaona, kwa sababu kwamba yeye alichukua misimamo hiyo mizuri mno aliyochukua, ambapo, mnajua, ufalme wake ulikuwa wa pili baada ya Sulemani. Alipanuka. Hata nchi zote jirani, zilimpenda, na—nao walilipa ushuru kwa ufalme wake. Pia tunaona ya kwamba, hata huko chini kabisa katika Misri, ushawishi wake ulitambulika. Na kwa kuwa huu ulikuwa ndio msimamo wake, naye nabii huyu kijana amesimama pale mbele ya huyu mfalme, yeye . . . Ulikuwa ni ushawishi mkubwa kwa Isaya, jinsi ambavyo Mungu angembariki mtu yeyote ambaye angekuwa mwaminifu kwa Neno Lake, haidhuru yale siasa zake ziliyojaribu kumshawishia, haijalishi vile kitu kingine chochote kilivyojaribu kuwa. Uzia alidhamiria kudumu na Neno, naye Mungu akambariki. Naye Isaya akaliona.

66 Hilo, kama kawaida, kama tu kundi la watu, kama tu tamshi nililosema kuwahusu Wafanyabiashara, wakati Uzia alipoanza kujisikia salama, ya kwamba alikuwa na karibu kila kitu katika huo ufalme ambacho Mungu alimjalia, alipata kiburi moyoni mwake.

67 Sasa, hilo ndilo ambalo limeyapata madhehebu yetu kote katika nyakati. Wanapojisikia kwamba wao ni wakubwa vya kutosha kusema, "Sasa, sisi ni *kile*," ndipo wanapata kiburi, na hapo ndipo Mungu anapowaacha. Na basi Wafanyabiashara wakifikia mahali hapo, ambapo tuna . . . Kama vile Ndugu Williams alivyosema, "Kumi na watano." Lakini Mungu anaweza kufanya mengi zaidi na kumi na watano mkononi Mwake kuliko angaliweza kufanya na elfu moja mia tano wasio mkononi Mwake. Mnaona? Lakini tunawathamini elfu moja mia tano mkononi Mwake badala ya kumi na tano mkononi Mwake, kama wote watadumu mkononi Mwake. Hilo ndilo jambo muhimu, kushawishiwa, sio kwa idadi kubwa tuliyo nayo, bali kwa Mungu mkuu tunayemwakilisha, na aina ya Uzima ulio ndani yetu kwa Yeye, ambao utawashawishi wengine.

68 Yesu alisema, "Ninyi ni chumvi ya dunia. Lakini chumvi

ikipoteza ladha yake, haifai tena kabisa; inatupwa nje, ikakanyagwa chini ya miguu ya watu." Kamwe haitupasi kusahau hilo. Sisi ni chumvi. Lakini chumvi ikipoteza nguvu zake, hiyo ni kusema, nguvu za—zake za kugusa. Nayo chumvi inaweza tu kuokoa inapogusa. Basi ikipoteza nguvu zake za kugusa, basi si chumvi tena, bali ni changarawe. Inafanywa ya kukanyagwa.

69 Basi tunapopoteza ushawishi wetu kama baba, kama mama, kama Mkristo, kama mfanyabiashara, kama mhudumu, tunapopoteza ushawishi wetu kwa watu! Sasa, tunaweza kuwa maarufu sana kwa njia ya ulimwengu, na kuendana na ulimwengu; bali ninamaanisha, kile tunachowakilisha, sisi tunamwakilisha Kristo. Tunapopoteza ushawishi wetu wa kuwa hivyo, kama kutokeza. . . Tunawezaje kushikamana na siku hizi wakati Mungu anazipinga siku hizi?

70 Mikaya angewezaje kusema, "Kwea ukafanikiwe. Ono langu liko moja kwa moja pamoja na lenu," wakati alijua kwamba Mungu alikuwa amewalaani watu hao waovu? Ono lake ilibidi liwe kinyume.

71 Nalo ono la mtu siku hizi, ambaye angeambatana na mkondo wa ulimwengu na bado abaki mhudumu, kuna kasoro fulani na ono la mtu huyo. Mnajua yale Mungu aliyosema kuhusu kanisa hili tajiri la Laodikia; lilimweka Yeye nje. Hatuwezi kusimama na imani ya watu wengi na kura ya siku hizi. Hatuna budi kukipinga kitu hicho. Sasa, kwa hiyo ni. . .

72 Mfalme huyu aliendelea vizuri mpaka akakuta kwamba mataifa yote yalikuwa yanamwogopa. Akapata idadi kubwa ya watu. Ufalme wake ukajengeka. Ndipo moyo wake ukajitukuza, kwa kiburi. "Mnaona, sisi ni ninii tu. . . Mimi ni mtu mkubwa sasa." Na hiyo ndiyo njia ya kutokea.

73 Njia ya kupanda juu ni kushuka. Unajuaje wapi juu ama chini? Maana, kama ulimwengu unasimama katika anga, unajuaje ni upi juu ama chini? Kwa hiyo, daima, "Yeye ajidhiliye, Mungu atamkweza. Yeye ajikwezaye, Mungu atamdhili." Yeye atamshusha chini. Dumu mnyenyekevu sikuzote, na uwe mdogo machoni pako mwenyewe. Haijalishi Mungu anakufanyia nini, angalia tu jinsi unavyoweza kuwa myenyekevu zaidi, wakati wote. Kadiri Mungu anavyozidi kukubariki, endelea tu kuwa mnyenyekevu zaidi, wakati wote. Yeye anaweza kuendelea kubariki.

74 Lakini unapofikia mahali, unawazia, "Ninalo," wewe huna. Uko njiani ukitoka. Hiyo ni kweli. Mnaona? Unapoteza ushawishi wako. Unapoteza ngu—nguvu zako za ushuhuda wako.

75 Wakati nyinyi wanawake mnapoanza kutamani kuwa kama wanawake wengine, kuna kasoro fulani. Wakati nyinyi wanaume, nyinyi wahudumu, wanapojaribu kujifananisha na

mtu mwingine, wakati nyinyi wafanyabiashara mnapojaribu kufanya biashara kwa kiwango ambacho mtu mwingine angeifanyia, kwa sababu wao wamefanikiwa. Sio sikuzote ufanisi unawakilisha fanaka katika Kristo, wakati mwingine ni kinyume sana. Mnaona?

76 Sasa, kiburi. Yeye alijitukuza, ndipo akawazia, "Mimi ni mtu mkuu jinsi gani!" Sana, alijitukuza, mpaka akajaribu kupachukua mahali pa mhudumu. Anaingia hekaluni, ambako alichukua, akatwaa chetezo cha moto, akaenda kwenye madhabahu ya uvumba. Sasa, hapo ni watu waliowekwa wakfu peke yao wangaliweza kufanya hivyo.

77 Sasa, kama nilivyosema hapo kabla, ndivyo nasema tena. Wafanyabiashara si wahubiri. Sisi wahubiri tuna wakati wa kutosha kujaribu kukinyosha Kitu hiki, achana na wafanyabiashara. Ninyi nyote ni wafanyabiashara, sio wahudumu. Basi usichukue mahali pa mmoja, au kujaribu kupachukua, kwa sababu hujaitiwa hilo. Mkitaka mtu fulani kuzungumza kwenye mikutano yenu mikubwa, mchukueni mhubiri, mtu aliyeitwa kufanya hivyo. Kwa sababu, mnaona harakati sisi wahudumu tulizo nazo. Na kwa hiyo mnaona mnalofanya.

78 Naye Uzia hapa, yeye alijaribu ku—kupachukua mahali pa kuhani. Aliwazia, "Vema, Mungu amenibariki. Kwa nini nisifanye hivyo?"

79 Kamwe usiingize hilo kichwani mwako. Mungu huita, na kuchagua tangu zamani, na kukusudia kimbele, kwa utukufu Wake. Hakuna kitu . . .

80 Mnakumbuka katika Biblia, hapo Musa alipokuwa akiwatoa Israeli kutoka Misri, wakivuka, kupitia, hadi kwenye nchi ya ahadi? Mnamkumbuka mmoja mle ndani, Dathani na wale waliojitukuza, na kusema, "Sasa, ngoja kidogo! Musa, unajaribu kuwa ndiwe msemaji wa pekee. Kuna watu wengine watakatifu miongoni hapa"?

81 Ndipo Mungu akasema, "Jitenge, maana nitawaangamiza."

82 Mungu alikuwa amechagua jambo fulani lifanywe, nalo halina budi kufanywa jinsi hiyo. Haitupasi kuingiza mawazo yetu wenyewe. Inatupasa kuheshimu wazo Lake na amri Yake.

83 Sasa, sio kurejea kwa dada zetu, lakini kwenye . . . Haijalishi mwanamke huyo mwingine anafanya nini, Mungu anacho kifananishio chako kimewekwa *Hapa*. Haijalishi mlei mwingine alifanya nini katika Biblia, Mungu anacho kifananishio chako hapa, jambo la kufanya. Tutalifikia, baada ya kitambo kidogo, labda, yale mlei anayopaswa kufanya, na mhudumu. Sisi sote tuna mahali petu, na hatuna budi kudumu katika wito wetu.

84 Sasa tunaona ya kwamba mtu huyu alijitukuza. Kwa hiyo akatwaa chetezo akaenda mbele madhabahuni, ambalo

liliruhusiwa tu, na Mungu, kwa watu waliowekwa wakfu kwenye wadhifa huo. Yeye alijaribu kupachukua mahali pa mhudumu.

85 Ndipo basi mhudumu akajaribu kumsahihisha. Tunaona ya kwamba makuhani themanini, mbali na kuhani mkuu, walimfuata na kumwambia. "Bwana," kwa maneno mengine, namna hii, "Mungu amekubariki. Wewe ni mtu mwenye heshima. Wewe ni mtu mashuhuri. Naye Mungu amekubariki katika kazi yako. Lakini ha—haikupasi kufanya hivyo. Unaiacha njia iliyowekwa."

86 Loo, jinsi ningeweza kusema mambo fulani hapa! Naam. "Kuondoka kwenye njia iliyowekwa." Lakini . . . Kwa kuwa kitu hicho ndivyo kilivyo, hebu tujaribu kuhifadhi tunachoweza kushika. Mnaona?

87 Yeye alisema, "Umepoteza njia, kwa kuwa Neno la Mungu linasema *hivi-na-hivi*. Kizazi cha Huruni pekee ndicho kitakachofanya hivi. Hiyo ni ya Huruni, na yeye pekee, na watoto wake. Kwa hiyo, ewe mfalme, tunakuheshimu. Tunakuenzi. Wewe ni mtu mashuhuri. Lakini usijaribu kufanya hivyo."

88 Naye je, alikuwa mnyenyekevu? La, bwana. Aliwazia, "Mungu amenibariki, kwa hiyo nitafanya tu nitakayo."

89 Sasa angalieni, ndugu zangu. Kuwa mwangalifu hapo. Kwa sababu, haijalishi Mungu amekujaza na Roho Wake kiasi gani, na yale umefanya, na jinsi ulivyobarikiwa vizuri, wewe dumu na wito wa Mungu. Usiende kando juu ya mapokeo fulani, na taratibu za kimadhehebu, na kadhalika. Afadhali urudi kwenye njia, afadhali urudi kwenye yale Mungu aliyoweka tangu mwanzo.

90 Sasa, kwa hiyo tunaona ya kwamba mtu huyu, wakati aliposahihishwa, badala ya kujinyeyekeza na kukubali kwamba Neno lilikuwa sahihi, na Mungu alikuwa amesema kweli, yeye alighadhabika. Kwa maneno mengine, yeye alikuwa tayari kumfukuza kwenye shirika lake. Alikuwa—alifadhaika sana kulihusu, akatatanika sana. Na, loo, akashikwa na hasira, na kama kugeuka na kusema, "Sasa, ngojeni tu kidogo. Hivi mnatambua mimi ni nani?"

91 Sasa, unaposahihishwa na Neno la Mungu, huna budi kulitii Neno. Basi akasema atafanya apendavyo. Yeye alikuwa ndiye kiongozi wa kitu hicho, kwa hiyo . . . angefanya tu apendavyo. Basi mnajua nini kilichotukia? Alipigwa kwa ukoma. Na huku hasira yake, ghadhabu ilipokuwa juu yake, kuhani akagundua ukoma usoni mwake.

92 Sasa, mnasema, "Vema, una maana gani?" *Ukoma* unawakilisha, ni—ni mfano, hasa, "wa dhambi." Na wakati mtu hatavumilia sahihisho kwa Neno la Mungu, yeye amejaa ukoma, analipuka na kufanya yasiyofaa. Unafanya kitu gani? Unafanya nini? Unauharibu ushawishi wako. Unaona? Jambo

fulani linatukia. Watu wanajua na wanaweza kutambua, lile Neno unalosahihiswa kwalo, ya kwamba hutafanya jambo hilo. Kwa hiyo unauharibu ushawishi wako.

93 Nalo lilimwudhi jamaa huyu. Hasira ilimpanda. Ndipo alipokuwa katika ghadhabu yake, ukoma ulikuwa usoni mwake. Nasi tunaona ya kwamba yeye. . .Sio kwamba tu alikiangusha chetezo, bali alikimbia kutoka kwenye nyumba ya Mungu, asiweze kurudi tena. Kwa sababu, haijalishi alikuwa ni mkuu jinsi gani na ushawishi mwingi kiasi gani aliokuwa ameupata, yeye. . .Hapo aliposahihishwa, basi alikataa kupokea sahihisho lake, kwa sababu hadhi yake katika jamii ilikuwa kubwa zaidi kwake kuliko vile Neno la Mungu lilivyokuwa. Nina hakika mnaelewa yale ninayoelekezea. Mnaona? Ilikuwa kubwa kwake. Wadhifa wake kama mfalme ulikuwa zaidi kwake kuliko Neno la Mungu.

94 Wakati shirika hili la Wafanyabiashara lifikapo mahali hapo, wakati mhudumu wa dhehebu lake anapofika mahali hapo, basi amekwisha. "Usizimie unapokemewa." Unaposoma jambo fulani katika Maandiko, nawe unajua ya kwamba inakupasa kujinyenyekeza na kulifuata Neno la Mungu, katika njia ambayo Yeye amekuchagulia ya kutembelea, halafu hulifanyi, basi, muda si muda wajua, umekwisha. Ushawishi wako umeharibika. Sasa, hatuna budi kukumbuka hilo.

95 Basi nabii huyu kijana, ni somo la jinsi gani hilo lilivyokuwa kwake! Ndipo alipomwona mfalme huyu, kwa jambo lili hili, Isaya alijifunza moja ya masomo yake makubwa kuliko yote. Kwamba, haidhuru mtu anaweza kuwa mkubwa jinsi gani, jinsi huenda ushawishi wake ukawa mkubwa, bali anapokosa kutembea katika Nuru, anapokosa kumtii Mungu, basi ushawishi wake unaharibika, naye anaondolewa hudumani.

96 Jambo lingine Isaya alilojifunza: alijifunza, kwa jambo hili, kwamba Mungu humweka mtu Wake mahali pake. Si wewe kujiweka mahali hapo, bali Mungu humweka mtu Wake mahali hapo. Hatuna budi kutambua hilo.

97 Mara nyingi nimetumia hili. Ninapenda kuwinda, kama mjuavyo. Huko juu Kaskazini, wakati—wakati majira ya baridi kali yanapoanza kuingia. Mabata wadogo huzaliwa huko juu, kwenye kidimbwi. Basi mara upepo huo mwanana wa kwanza unapoifunika milima, na vipande vidogo vya theluji vinaanguka. . .Sasa, maskini bata huyo aliyezaliwa katika msimu wa Kuchipusha majani, huko juu kwenye ziwa hilo, naye kamwe hajawahi kuondoka humo ziwani. Yeye hajui chochote kuhusu kitu chochote kingine ila ziwa hilo. Lakini hakika tu kama upepo huo mwanana unavyovuma, naye anauhisi upepo huo mwanana ukivuma, yeye hukimbia moja kwa moja hadi katikati ya huo, anaogelea huko nje, na kuinua maskini pua yake juu hewani, na kutoa mlio mara chache. Na kila bata kwenye

kile kidimbwi atakuja kwake moja kwa moja. Naye atasimama, akiwa na silika hiyo ndani yake, akijua kwamba hivi karibuni kidimbwi hicho kitagandamana kabisa, ama ziwa. Naye ataenda moja kwa moja hadi Louisiana awezavyo kwenda. Ataenda.

98 Kwa nini? Kuna kitu fulani ndani yake. Ni silika iliyotolewa na Mungu, naye anaitumia. Inamwongoza. Sasa, inafanya nini? Vipi kama alienda . . . Kama silika hiyo ilimwongoza mbele zaidi kaskazini, basi angejua kulikuwa na kasoro fulani. Nao hao mabata wasingemfuata, kwa sababu anaenda kinyume na njia ya kawaida.

99 Basi tunapofikia mahali ambapo tunajaribu kuwaongoza watu kinyume, wao wanasema, "Vema, sisi, Wamethodisti, tunalo. Sisi, Wabaptisti, tunalo." Hilo silo.

100 Mungu analo. Mnaona? Hiyo ni kweli. "Na hapo mwanzo alikuwako Neno, naye huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Naye Neno angali ni Mungu. Kwa hiyo Mungu ndiye aliye nalo. Basi hebu tuelekee njia hiyo, kwenye mapito ya kawaida, na tusijaribu kuelekea njia nyingine.

101 Halafu basi tunaona ya kwamba maskini bata huyu, kwa kuwa yeye alikuwa . . . Hakuna yeyote wa hao mabata wengine aliyeonekana kuwa na lolote, lolote ila "amina." Kwa sababu, kuna jambo fulani kumhusu maskini jamaa huyo walilolijua, jinsi, huo mlio, baragumu hiyo aliyoipiga. Wa—walijua ya kwamba yeye alikuwa na ile kweli.

102 Na kuna jambo fulani kuhusu Injili, pamoja na nguvu za ufufuo wa Yesu Kristo. Paulo alisema, "Baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani atakayejua jinsi ya kujiandaa kwa ajili ya vita?" Sasa, ila Injili inapotoa sauti, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele," nasi tunaiangalia na kuona kwamba ni Kweli, na iko pamoja na Neno, hilo ndilo jambo linalomshawishi bata halisi.

103 Sasa, kunao wengine kwenye hicho kidimbwi, kama kanga wa majini na kadhalika. Wanayo njia nyingine; kuku wa matopeni na wote kama hao; bali wanadumu na njia yao wenyewe. Lakini bata halisi huendelea. Mungu alimweka maskini bata huyo hapo na kumpa hiyo, kwa kuwa Mungu alimweka apate kuwa hivyo.

104 Na sasa, "Mungu ameweka, Kanisani . . ." "Mungu," sio dhehebu, sio mafanikio ya mwanadamu, kufanya maaskofu na kadhalika, wazee wa jimbo. Lakini, "Mungu ameweka, Kanisani, kwanza mitume," hao ni wamishenari, "pili manabii, walimu, wachungaji, wainjilisti." Mungu aliwaweka Kanisani, na kila baragumu italia vile vile, Injili ile ile. Mnaona? Kama yeye ni nabii, yeye hupiga baragumu ya nabii. Anatabiri mambo yajayo, na yanatimia kila wakati.

105 Sasa, msichana mdogo alinijia hivi majuzi. Huenda yupo hapa ameketi sasa. Naye akasema, "Ndugu Branham, nilikupa

ndoto. Na katika ndoto hii ni—nilikuwa na kitu fulani. Na—nataka uniambie." Nikaketi chini. Sasa, kama kunaye aliye nje, hapa ndani, nje ya milki za Kipentekoste, hebu niwaombe radhi, kwa dakika moja.

Ndipo akasema, "Kamwe hukuniambia ndoto yangu."

106 Nikasema, "Kipenzi, keti chini kwa dakika moja." Ndipo nikasema, "Baba na mama yako ni marafiki wangu wazuri sana, wakulima waliostaafu ambao walitoka mbali sana, kuja kuishi pamoja nasi." Kisha nikasema, "Wa—wao wananiamini, kama mtumishi wa Kristo. Wewe ni mtoto tu yapata umri wa miaka kumi na miwili." Nafikiri yeye huenda shuleni na Becky wangu.

107 Ndipo nikasema, "Tazama, utakutana na mambo mengi sana huku nje, kipenzi, katika jina la Ukristo." Nikasema, "Ukimpata mtu aliye na kila fasiri, *hivi* tu, [Ndugu Branham anadata vidole vyake mara kadhaa—Mh.] ana kila, namna *hiyo* tu, katika Jina la Bwana," nikasema, "kuwa mwangalifu kuhusu hilo. Hilo ni kinyume na Maandiko."

108 Yesu alisema kulikuwako wenye ukoma wengi katika siku za Eliya, bali ni mmoja tu aliyetumwa kwake. Mmoja. Wajane wengi katika siku za Elisha, bali alitumwa kwa mmoja tu. Mambo mengi ambayo Yesu hakufanya, mara nyingi.

109 Hivyo vitimbi vilivyo na kila jibu, kuwa mwangalifu. Mtu anaposimama na kunena katika Jina la Bwana, hayo sharti yawe ni kweli. Hayana budi kuwa ni kweli kabisa.

110 Huenda ikawa, niani mwako, umepata dhana. Nikasema, "Sasa, kipenzi, ninaamini ningeweza kukwambia ninavyofikiria ndoto yako ilivyo. Ila kukwambia, katika Jina la Bwana, la, bwana."

111 Maana, yeye anayajua hayo mambo. Nikasema, "Hivi nimewahi kunena nanyi katika Jina la Bwana ila lile lililotukia?" Nikasema, "Maelfu wamekuja, na kusema *hivi, vile*." Nikasema, "Siwezi kukwambia ndoto yako ni nini mpaka niione tena, na halafu Yeye ananiambia, ndipo ninaweza kusema, 'Bwana aliniambia.' Mpaka wakati huo, sijui mimi. Sitaki kuchukua ushawishi wangu mwenyewe na maoni yangu mwenyewe. Siwezi kusema BWANA ASEMA HIVI, kwa kuwa huyo ni mimi nikiliwazia; hilo ni zuri sana, kwa maoni yangu."

112 Hatuna budi kuwa waaminifu, kwa sababu tunacho kitu kilicho kikuu kuliko vyote ulimwenguni. Hazina ya Mbinguni iliyo kuu zaidi ni Kristo miongoni mwetu. Kwa nini tunataka kibadala cha maskini ushawishi fulani, kujaribu kujifanyia wenyewe mtu fulani mkubwa miongoni mwa mtu fulani hapa? Kwa nini tusiwe mtumishi mnyenyekevu kwa Kristo?

113 Nami nikasema, "Hiyo ndiyo sababu ninaweza kuwaambia habari za Biblia." Nikasema, "Kama nilikwambia tulikuwa tu

tukienda Arizona. . .Nadhani mama na baba yako wanaenda, kwenye mkutano mkubwa wa Wafanyabiashara."

Akasema, "Wanaenda."

114 Nikasema, "Vipi kama nilikwambia, usiku wa kwanza, 'Nilikwambia sasa, katika Jina la Bwana, ya kwamba kungekuwako na mwanamke atakayeingia, kilema, naye angekuwa *hivi*,' kama ulivyolisikia likisemwa? 'Na kisha mwanamke huyo, ambaye amelemaa kwa miaka mingi sana, mara baada ya maombi yeye atasimama na kuondoka.'"

115 Nikasema, "Vipi kama ningekwambia basi, 'Katikati ya huo mkutano, mama fulani aliyekuwa na mtoto mchanga kichwamaji, na mara tulipoomba, kichwa cha mtoto huyo kikawa kawaida'? Kwamba, 'Mwishoni mwa huo mkutano, kungekuwako na watu wanne waliombeba mtu ambaye alikuwa amekufa kwa siku *kadhaa*.' Walikuwa wamemleta. 'Walikuwa wamevaa suti nyeusi,' na nitoe sifa zao. Basi mara nitakapomwomba Baba yetu wa Mbinguni, roho yake ingemrudia." Ndipo nikasema, "Ambalo, unajua, limetukia."

116 Sasa, nikasema, "Ndipo ningesema, 'Ndugu yako mdogo,'" yeye ni maskini mtoto wa miaka mitano. Kisha nikasema, "Vipi kama akiuawa mtaani? 'Naye atauawa, nawe utamleta kwangu. Nami nitakuwa nimesimama karibu na ki—kipandio cha mlango, ambapo pana mtu mwenye suti nyepesi. Nitakuwa nikizungumza naye. Ndipo maskini ndugu yako ataponywa.'"

117 Sasa nikasema, "Basi kama hilo lilitukia, vipi kama ulienda pale nje basi, na huyo mwanamke, akiwa na baridi yabisi ama chochote kilichokuwa, mwanamke aliyelemaa, hakuwako? Vipi kama mtoto huyo kichwamaji hakuwapo? Basi umechanganyikiwa kabisa niani mwako. Hujui. Nami nilizungumza nawe na kukwambia 'BWANA ASEMA HIVI.'" Nikasema, "Basi ushawishi wangu umepotea. Huenda ukanihitaji siku moja, vibaya sana."

118 Nikasema, "Lakini vipi kama huyo mwanamke yupo hapo? Vipi kama mtoto huyo kichwamaji ameponywa? Vipi kama mtu huyo akifufuliwa katika wafu? Basi, maskini ndugu yako akiuawa, hata hutalia. Ungesema, 'Baba, hebu nimchukue. Nitakuonyesha utukufu wa Mungu.' Kwa nini? Ilikuwa ni kweli, *hapa*. Ilikuwa ni kweli, *pale*. Ilikuwa ni kweli, *pale*. Ilikuwa ni kweli, *pale*. Kila wakati, ni kweli, basi unajua ni kweli." Nikasema, "Hiyo ndiyo sababu tunataka kuliamini Neno la Mungu."

119 Katika bustani ya Edeni, ilinenwa juu ya Masihi atakayekuja, kama Mwokozi. Manabii waliliona kimbele. Yeye alikuja vile hasa Biblia ilivyosema.

120 Nebkadreza aliota ndoto, naye Danieli akaifasiri, yeye, juu ya falme za Mataifa, kikamilifu, kila wakati.

121 Na kila kitu Biblia imewahi kunena habari zake, Biblia inakisema *hapa*; historia inasema kilitukia. Biblia ilisema *hapa*, historia inasema kilitukia.

122 Sasa, tuko katika wakati wa Kunyakuliwa. Itatendeka. Kwa sababu imekuwa ni kamilifu, kila wakati mwingine, haina budi kuwa kamilifu wakati huu. Mungu anawaita watu, mnaona, na ndio ule wakati. Hatuna budi kuwa waaminifu.

123 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . Bwana. Sasa, una kitu fulani, bali kuwa mwangalifu nacho. Utaangamiza ushawishi wako ikiwa kitu hicho hakitatimia. Mnajua ninalomaanisha? [Kusanyiko linasema, "Amina."] "Loo," mnasema, "Mimi ni mfuasi . . . " Sijali wewe ni mfuasi wa wapi, ndugu, dada. Halina budi kutukia jinsi hasa ulivyolisema. Kama sivyo, umejifanya tu kitu cha kuchekwa. Umejiletea tu fedheha, ukauangamiza ushawishi wako, na kuangamiza ushuhuda wa Yesu Kristo unaoubeba. Kuwa mwangalifu. Sasa, fundisho lako juu ya mambo hayo ni sawa. Bali linaambatana na ahadi na chini ya masharti, kwa hiyo kuwa mwangalifu kuhusu ushawishi wako. Hapa, Mungu . . .

124 Wakati mwingine tunakuta kwamba mtu fulani alinena kwa lugha. Huyo mwingine anataka kumwiga; yeye atanena kwa lugha, pia. Mmoja anamwona mwingine akitoa fasiri; huyo mwingine anasema, "Ninayo, pia." Nawe unaenda kwa dhana, kisha unasema, "BWANA ASEMA HIVI." Vema, hilo ni kosa. Na Mungu kamwe hatawasogeza mbele zaidi, kile mlicho sasa hivi, dhehebu tu, mpaka mtoke kwenye hilo.

125 Sasa, huenda msinipende sasa. Bali kwenye Siku ya Hukumu, mtanipenda. Mnaona?

126 Kuwa na hakika. Kamwe usiliseme isipokuwa Mungu amesema hivyo, nawe unajua ya kwamba ni kweli, kwamba Mungu alisema hivyo. Sio maoni yako, bali si dhana fulani; kwa sababu, unaweza kuwa na dhana kwa njia yoyote.

127 Hao manabii kule chini, wakati Yehoshafati na—na Ahabu walipokuwa wameketi malangoni, hao watu walikuwa waaminifu, nao walikuwa wamevuviwa. Lakini, mnaona, uvuvio wao haukuambatana na ahadi ya Biblia. Maana, nabii Isaya . . . Samahani. Nabii aliyetabiri mbele yao, Elisha, Eliya, na kumlaani Ahabu na Yezebeli, na kusema yale yangewapata. Kwa hiyo baraka hii ingewezaje kuwa juu ya kile Mungu alikuwa amelaani?

128 Nayo baraka inawezaje kuwa juu ya watu wanaofanya na kutenda jinsi Mungu alivyosema isitendwe? "Hata tukicheza katika Roho, hata tukinena kwa lugha za watu na za malaika, wala hatuna upendo, inakuwa kama shaba iliayo ama upatu uvumao."

129 Sasa, mnayo ile Kweli, bali inawabidi kuijia kitofauti na sha—shangwe kubwa tu, mnajua ninalomaanisha, kitu tu cha

kupigia makelele. Nami ninaamini katika kupiga makelele kukihusu, kikiwa na kitu cha kupigia makelele. Lakini iweni na hakika ya kwamba mnakiendea hicho kwa kilindi chenyewe cha uaminifu. Kama ukiishi maisha tofauti na yale unayopaswa kuishi, kaa kimya mpaka utakapoupata huo Uzima; uanze kuishi ndani yako, basi, wenyewe.

130 Mwajua, kondoo haombwi kutengeneza sufu. La. Yeye hawezi kuitengeneza. Karama hizi haziwezi kutengenezwa kwa mhemko. Kanisa hili haliwezi kuundwa na dhehebu. Kondoo hutoa sufu kwa sababu yeye ni kondoo. Hawezi kujizuia kutoa sufu, kwa kuwa mfumo wake wote umefanywa upate kutoa sufu. Hatuna budi kuwa kile tulicho ndani, sio kitu fulani nje.

131 Tunawezaje kujua yaliyo sahihi, kisha tuzungumze kinyume? Hivi Yesu hakusema, "Enyi wanafiki! Mwawezaje kusema mambo mazuri, wakati, kutoka kwa wingi wa moyo, kinywa hunena?" Mnaona? Hatuna budi kuwa na hakika kwamba tunaposema mambo haya, kwamba ni sahihi.

132 Sasa, kuharakisha. Nami sina budi kuharakisha, kwa kuwa nadhani nimechelewa kupita kiasi sasa. Mtanivumilia kwa dakika moja tu zaidi? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Naam.

133 Isaya alijifunza papa hapa. Haijalishi shirika lilikuwa kubwa jinsi gani, jinsi huyo mtu alivyokuwa mkuu, ingawa Mungu alikuwa amempa maelfu na mamilioni ya dola za wakati huu tunaoishi, hilo halikumaanisha kitu kimoja mbele za Mungu. Neno Lake lilikuwa . . .

134 Neno Lake ndilo yakini Yake, na hilo latosha. Huna budi kulitii Neno Lake. Jinyenyekeze, na Hilo.

135 Angalieni. Ndipo tunaona ya kwamba yeye alifanya jambo fulani kinyume na Neno, naye akalaaniwa kwalo, haijalishi alikuwa ni mkuu jinsi gani.

136 Jinsi Daudi alivyokuwa mkuu, mtu aliyeupendeza moyo wa Mungu, hata hivyo akaondoka kwenye Neno, "Usizini."

137 Lakini Daudi alijitukuza. Akafikiri, "Vema, Mungu halijali jambo hili." Mungu hujali kila wazo unalowazia. Mawazo yako na yawe mazuri kabisa. Shida ilikuwa ni nini? Sasa, ni kwa sababu alisahau hilo. Alisa- . . . Aliliondokea. Kamwe hakulisahau, maana aliambiwa vema zaidi.

138 Sasa, Mungu humweka mtu Wake mahali fulani, Naye hatakubali pengine. Hakuna mtu anayeweza kupachukua mahali pa mtu mwingine.

139 Ndugu Green hapa, dakika chache zilizopita, ule muziki. Mimi—mimi . . . Muda mrefu tangu nilipomsikia Ndugu Green, na huo uliuchangamsha sana moyo wangu, mtu mzuri.

140 Lakini nilikuwa nikisoma, katika siku za Bibi McPherson, wakati nilipoona baadhi ya mambo yaliyotokea. Bibi McPherson

alikuwa—alikuwa mwanamke mwenye ushawishi, bali niliona ya kwamba kila mwanamke mhudumu ilibidi abebe Biblia yake kama tu Bibi McPherson. Loo, jamani!

141 Na sisi—sisi tunaona jambo lile lile, kunao Billy Graham elfu kumi leo hii. Hivi mlipata kuwaona, wakijaribu kuzungumza tu kama yeye?

142 Wewe kuwa kile ulicho. Dumu jinsi ulivyo. Huwezi kuwa Billy Graham, wala Billy Graham hawezi kuwa wewe. Mahali pako ni muhimu tu kama Billy Graham. Kama unashughulikia umaarufu wa ulimwengu, huenda ukajaribu kuiga; hutafikia popote katika Ufalme wa Mungu. "Afadhali niwe mkeka wa mlangoni kwenye nyumba ya Mungu." Dumu na kile ulicho, kile Mungu alichokufanya. Loo! Jinsi tungeweza kusema . . .

143 Sababu ya wao kufanya hivyo, ni kwa sababu hawatambui kwamba Mungu anawatazama. Mnaona? Unapoteza wazo lenyewe la Mungu kuwa hapo, akikusikiliza. Mungu anaandika kila kitu unachowazia. Naye anajua, katika kitabu Chake cha kumbukumbu. Mawazo yako yana sauti kubwa Mbinguni kuliko sauti yako duniani. Wazia jambo jema.

144 Kama nilivyomwambia mtoto Joseph, nilisema, "M—mvulana mdogo huzaliwa katika ulimwengu huu, anasimama moja kwa moja katikati ya hiyo barabara, naye anaelekezwa Kalvari, kwa Kristo. Kunao mti kila upande wa barabara. Mmoja mkono wa kushoto, ambao nitauita 'mabaya,' kama akianza tu kuwapiga wavulana wadogo makofi usoni kwa sababu walimpiga. Basi wakianza kufanya mambo haya, inamvuta mvulana huyo mdogo, kwa ushawishi, na kumfanya mpotovu. Lakini kama akiuchukua upande huu mwingine wa barabara, ambao ni Roho Mtakatifu, Yeye humwelekeza moja kwa moja Kalvari, na kumdumisha hivyo. Inakufanya ukue umenyooka. Mawazo yako, ni rahisi tu kuwaza mawazo mema kama ilivyo kuyawaza mabaya. Rahisi tu kuwazia mema juu ya wale wanaokuwazia maovu, kama ilivyo vinginevyo. Na, vema zaidi, itakufanya ukue umenyooka." Unaona? Kaa mnyofu kwa Mungu.

Sasa, kuharakisha.

145 Lile ono hekaluni, yeye alimwona Mungu juu ya kiti Chake cha enzi, ameinuliwa. Loo, angalieni *Serafi* wa Mbinguni, ambalo linamaanisha "wateketezaji," Mtu maalum aliyeteuliwa. Wakati Isaya huyu aliposhuka kwenda hekaluni, alikuwa akiegemea begani mwa—mwa Uzia, na popote mfalme alipoenda. Yeye . . . Lakini akakuta kwamba, wakati mfalme, haidhuru alikuwa ameshawishika jinsi gani, alikuwa na ushawishi kwake, na mambo aliyokuwa amefanya, yaliyokuwa ni makuu, alikuta kwamba, wakati alipojaribu kupachukua mahali pa mwingine, alishindwa.

146 Tunayo mengi sana siku hizi, ya uigaji wa kimwili. Inafanya nini? Hebu—hebu nichukue . . .

147 [Kusanyiko linasema, “Ni sawa. Vema. Endelea nayo, ndugu.”—Mh.] Niendelee? Vema. Asanteni.

148 Angalieni, siku hizi, Mungu hutuma kitu fulani duniani. Nasi tunapofanya hivyo, kunafanyika nini? Kila mtu hana budi kuwa vivyo hivyo.

149 Si muda mrefu uliopita walimleta maskini mvulana wa Kipentekoste huku, jina lake maskini David Walker. Naye mvulana huyo mdogo alikuwa ni mhubiri. Nimewasikia wavulana wadogo wakisema, “Mtoto mdogo Yesu, aliyezaliwa katika ho- . . . Mama, hilo lingine lililikuwa ni nini?” Mnaona? Bali si maskini mvulana huyo. Nilienda kumsikiliza. Alitupa koti lake, kisha akachukua somo, na akalishughulikia kama kasisi. Lakini, ninaamini alikuwa mfuasi wa kundi la umoja.

150 Vema, sasa, kundi la utatu halitatetea—halitalitetea hilo. Nitawaambia hilo. Kwa hiyo wakajitwalia David mdogo. Basi mvulana huyo mdogo alipofika Florida, alinipigia simu nishuke kule nikamsaidie. Nami nikachukua ukurasa wa mbele wa gazeti, nao iliwabidi kuweka sehemu ya ziada ndani yake kwa ajili ya maskini akina David: mvulana mdogo, wasichana wadogo, maskini watoto wenye umri wa miaka mitatu, umri wa miaka miwili, kila mtu akijaribu kulishikilia kundi lao dogo pamoja. Inaonekana kwangu kana kwamba imekuwa ni tikiti ya posho ya Kipentekoste.

151 Kama hao ndugu wote wangalimzunguka maskini mvulana huyo na kumtunza, wamwombee, na kadhalika, kwamba asijitukuze, na kumtuma kwenye makundi hayo yote, na kumfanya aliweke fundisho la—lake kwa nafsi yake, lakini aendelee tu na kuhubiri, na kwa ajili ya wote, angaliwaleta maelfu ya watoto wadogo.

152 Lakini waliibua maigizo madogo, nao ulimwengu wa nje ukaingia hapa ndani. Walisikia juu ya David mdogo, naye huyu hapa mmoja aliye mkuu kuliko maskini David, kwa hiyo wakaja karibu na kuliangalia. Na kusema . . . Vema, wanaingia kule na kuona mwanguko mkubwa kabisa, kwa hiyo basi wanarudi na kusema, “Haya basi.”

153 Wanapomsikia mtu fulani akinena kwa lugha na kutoa fasiri, kasema, “Bwana atafanya jambo fulani,” na kuliona likitukia vivyo hivyo tu.

154 Kisha wanaenda kwa lingine, nao wanaona lundo tu la uigaji likirudi. Wanaenda huku na huku, wanasema, “Ninyi nyote ni wendawazimu.” Mnaona, ni kujilinganisha kimwili. Msifanye hivyo.

155 “Wale wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya.” Jalia nikinyenyekeze kiburi changu, na kuliita tu Jina Lake. “Jalia

ningojee, Bwana.” Iwapo kamwe hatafanya zaidi kwangu ila kuniokoa, hilo ndilo ninalotaka. “Iwapo ulikuwa na haja nami, nionyeshe, na ili kwamba nijue, ndipo nitaenda. Lakini Wewe niambie, kwanza. Nipo hapa, mtumishi Wako.” Fanya hivyo na ushawishi wako utakuwa mkubwa. Angalieni, Mungu ni Mtakatifu kabisa.

156 Nabii huyu alikuwa akiegemea juu ya mikono ya mfalme huyu. Lakini wakati alipokuta kwamba jambo fulani lilitukia. . .Haijalishi mtu alikuwa amebarikiwa kiasi gani, hata hivyo wakati Mungu. . .yeye anavuka mpaka huo kati ya kosa na ukweli, Mungu anamwajibisha. Ndipo Isaya akashuka hekaluni akaanguka magotini mwake. Hapana shaka alikuwa amesema, “Naam, mheshimiwa mfalme! Mtukufu, bwana,” na kadhalika, bali i—ilikuwa. . .ama “Jalali, bwana.” Ingalikuwa ni tofauti sasa.

157 Yeye alianguka chini hekaluni, madhabahuni, akaanza kulia. Na wakati akilia, Mungu akashuka chini katika ono. Naye akawaona Malaika wakienda huku na huko hekaluni, mabawa juu ya miguu Yao, na mabawa juu ya uso Wao, wakiruka, wakiitana, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana Mungu Mwenyezi.”

158 Naye akasema, “Nilimwona Mungu ameinuliwa juu,” juu sana zaidi ya mtu yeyote hapa duniani, juu ya Sulemani, ama Daudi fulani, ama Uzia. Mungu alikuwa ameinuliwa hadi mahali ambapo mwanadamu hawezi kuja, ndipo akashawishiwa kwa njia nyingine. Alimwona Mungu ameinuliwa, juu, juu sana, na pindo la vazi Lake. Basi alipowaona hao wenye Uhai wenye nguvu, mahali hapo palijaa moshi. Ndipo akaangalia, nazo nguzo za hekalu, mihimili, ikaanza kutikisika kwa sauti Yao. Hakuona hilo kwa Uzia. Yeye aliona kwamba mtu anayepatikana na mauti anaweza kuanguka. Haijalishi amebarikiwa kiasi gani, angali anaweza kuanguka. Lakini alimwona Mmoja asiyeweza kuanguka, ambaye misingi yake ni imara, hata nguzo za hekalu zilitikisika kwa sauti Zao.

159 Wazia jambo hilo. Mabawa mawili, walizifunika nyuso Zao. Wazia, hata Malaika huzifunika nyuso Zao takatifu. Hao Maserafi, wao ni wa pili kutoka kwa Makerubi. Wao ni sawa na Makerubi. Wao ni wateketezaji dhabihu. Na hiyo ni kuwafanya, wa—watoto, waabuduo mle ndani kabisa, wakiwahakikishia njia. Nao Maserafi hawa, wanaokaa Uweponi mwa Mungu, inawabidi kuzifunika nyuso Zao.

160 Halafu tunalichukua tu Jina la Mungu na kulitumia kwa njia yoyote, tunatabiri Kwalo, wakati haimaanishi kitu ila namna fulani ya ushawishi wa kimwili na kadhalika, na kusema mambo ambayo kamwe hayatimii, na kutenda kana kwamba haijalishi kabisa. Kama ukisema jambo fulani, na kwa uaminifu,

wala halikutimia, tubu na uliseme, kwamba ulikuwa umekosea. Ndipo ushawishi wako utarudi, huyo mtu ni mwaminifu.

161 Malaika hawa, Maserafi, kamwe hawakujua dhambi wala chochote kuhusu dhambi. Wanateketeza tu dhabihu, kufanya njia kwa ajili ya mwabuduo, watakatifu. Nao inawabidi kuzifunika nyuso Zao. Hiyo ingekuwa nini, juu karibu na Uzia? Kuzifunika nyuso Zao takatifu, Mbele za Mungu, kwa uchaji.

162 Sasa hakuna uchaji. Inaonekana kana kwamba tunaweza tu kufanya lolote, katika Jina la Bwana, na kupita nalo. Mradi tu sisi ni wafuasi wa kundi fulani lililo na nafasi nzuri ya kijamii, nao hawatunyang'anyi makaratasi yetu; wazee wa jimbo na maaskofu, na kadhalika, hawayatwai makaratasi yetu, nasi tungali tuna ushawishi mzuri miongoni mwa watu.

163 Lakini tuna ushawishi wa namna gani Mbele za Mungu? Hivi maombi yetu hurudi bure, ama yanajibiwa? "Mkikaa ndani Yangu, nalo Neno Langu likae ndani yenu, ombeni mtakalo nanyi mtatendewa. Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya. Hata nyingi kuliko hizi atafanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba."

164 Tuko wapi, enyi Wapentekoste? Tunajikuta kwenye ramani ya barabarani, asubuhi ya leo. Hebu tusipitwe. La, bwana. Kuna njia moja iendayo Mbinguni, na hiyo ni barabara ya utakatifu. Wenye haki hutembea ndani yake. Asiyeamini huicheka. Inategemea kile ulicho.

165 Sasa, watu hawana uchaji. Nao wale wanaojaribu kuishi vema, baadhi yao ambao wanapaswa kuwa wakiuheshimu msimamo huo ambao huyo mtu ameuchukua, ama mwanamke ameuchukua, wanawacheka.

166 Mwanamume, hivi majuzi, kwa kuwa mwanamke mmoja alikuwa amevuta nywele zake nyuma na kufanya fundo mviringo nyuma yake, alichukua Isaya 5, na kusema, "Zikate hizo nywele zote," kasema, "kwa sababu Hiyo ilisema, 'matairi ya mviringo.'" Mtu yeyote asiyejua mengi juu ya Neno la Mungu kuliko kiasi hicho, wakati Neno la Mungu lilisema ni fedheha, aibu, jambo la aibu, kwa mwanamke kuzikata nywele zake. Kasema, "Toa pumzi tairi lako, tairi la spea, utahudhuria kanisa hili," nao wanawake wakimcheka. Kwa sababu, haya basi. Hakuna uchaji! Hawalijui Neno! Hawaliheshimu Hilo wakati wanapoambiwa Hilo! Wahudumu huliona Neno la Mungu na kukataa kutembea ndani Yake.

167 Inanikumbusha, nikishuka kuja huku, nilikuwa na moja ya hizi hapa kamera. Na hiyo—hiyo kidogo ni kitu kipya, kwangu. Billy huitumia, vizuri sana. Nayo ina moja ya hivi vitafuta umbali, chochote ilicho. Nami nikaangalia kupitia kitu fulani, nikaona vitu vitatu ama vinne, navyo vyote vilionekana vinafanana kabisa. Nikasema, "Hiyo haiwezekani." Nikaangalia *hivi*, nami nikaona kimoja tu. Kisha nikaangalia *hivi*, tena

nikaona vitatu ama vinne. Nikashika kitu hiki kidogo na kukiweka fokasi mpaka vikawa kimoja.

168 Hilo ndilo kanisa linalohitaji, kitafuta umbali. Tumia kitafuta umbali chako. Ni kitu gani? Hii *hapa*. "Kwa kuwa kila atakayeliondoa Neno moja Kwake, au kuongeza neno moja Kwake, huyo ataondolewa, sehemu yake, katika Kitabu cha Uzima." Kitafuta umbali chako. Una vitatu ama vinne, hujui la kufanya nacho, ivute iwe Kimoja. "Mungu ni Mmoja." Neno Lake ni moja. Watu wake ni wamoja, sio madhehebu elfu tano mia sita na sitini na sita. Wao ni mmoja, mmoja tu. "Siku hiyo, mtajua ya kwamba Mimi ni ndani ya Baba, Baba ndani Yangu; Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu." Kweli. Chukua kitafuta umbali chako, kivute ndani.

169 Hakuna uchaji. Watu wanajaribu kufanya haki. Watu huchukua msimamo kwa ajili ya Neno la Mungu na kusema, "Nitalisafisha kusanyiko langu." Kitu cha kwanza unajua, malalamiko yanaingia ndani kutoka kwa mtu mwingine, nao wanamfukuza. Hana budi kutoka aingie mtaani. Kwa nini? Hawajashawishika kuhusu Uwepo Wake.

170 Unapaswa kufanya kama Daudi alivyosema, "Namweka Bwana daima mbele za uso wangu. Sitatikisika. Bwana na awe mbele zangu. Nitakuwa na Yeye kwenye mkono wangu wa kuume sasa. Atakuwa mbele ya uso wangu."

171 "Popote nionapo, ninataka kumwona Yesu ndani yake. Sitaenda mahali popote; sitafanya lolote; ushawishi wangu, jalia tu uwe kwa ajili Yake." Basi kitafuta umbali chako kimeipata ile Kweli. "Kwa kuwa kama Uzima wa Kristo. . . Nia iliyokuwamo ndani ya Kristo na iwe ndani yenu."

172 Na Yeye sikuzote alikuwa kwenye Neno la Baba, kufanya kazi Yake. Kasema, "Ni nani kati yenu anayeweza kunishtaki Mimi kwamba nina dhambi, kutokuamini? Kila kitu Biblia ilichosema kwamba ningekifanya, nilikithibitisha. Mungu amekithibitisha kupitia Mimi, kwamba Mimi ndiye Masihi. Ni nani kati yenu anayeweza kunishtaki Mimi kwamba nina dhambi? Mpaka mnapoweza kufanya mambo nifanyayo, na kulifanya Neno lithibitishe, kwenu, kwamba Neno limethibitishwa na Mimi, basi tulieni. Kwa sababu, dhambi ni kutokuamini katika Neno la Mungu. Yeye asiyeamini amehukumiwa tayari." Mnaona? Loo! Mahali ambapo tumesimama, enyi kanisa, ni wapi?

173 Sasa, Wao walikuwa na mabawa mawili juu ya nyuso Zao. Hiyo ilikuwa ni nini? Unyenyekevu katika Uwepo Wake.

174 Musa alivua viatu vyake, katika Uwepo wa Mungu. Paulo alianguka chini, kuibusu ardhi, tuseme. Alikuwa Uweponi mwa Mungu. Yohana Mbatizaji alisema, "Sistahili hata kuvifungua viatu vya miguu Yake."

175 Mabawa juu ya miguu Yao, unyenyekevu, wakiangalia wanapokanyaga, yale wafanyayo, wakitambua Wako kwenye mahali patakatifu. Loo, laiti tungalifanya hivyo, kamwe tusingetembea katika . . . sehemu hizi zisizofaa. Kamwe tusingeyafanya mambo haya, na yaliyo mabaya.

Sasa angalia. Sikuzote sikilizeni. Tambua udogo wako.

176 U nani wewe? Ingiza kidole chako kwenye ndoo ya maji na kukitoa, kisha tafuta shimo ulimoingiza kidole chako. Kisha useme, "Huyo alikuwa ni mimi." Wewe si kitu. Hutakumbukwa baada ya, muda mfupi baada ya wewe kuondoka. Wana msafara wa mazishi hapa nje, na ni hayo tu. Lakini ushawishi wako utaendelea kuishi, na kuendelea, na kuendelea.

177 Hiyo ndiyo sababu leo hii, katikati ya makafiri, kamwe hawajawahi kuelezea na kupata njia ya kuuondokea ushawishi wa Mtu mmoja, Yesu Kristo, Yule aliyekuwa ni Mungu aliyefanyika mwili. Wakati alipoutoa uhai Wake huku chini duniani, ulifanya mahali pa kufyonza ambapo huwavuta watu wote Kwake, katika ule mzunguko mkuu wa maisha Yake yaliyokuwa duniani wakati mmoja. Huwezi kuukaribia pasipo kuingizwa ndani yake.

178 Lakini, mimi na wewe, sisi si kitu. Sisi si kitu. Hebu tuwazie ni kitu gani kinachotuvuta. Mimi . . . Mtumbwi wangu mdogo, juu ya bahari ya wakati, haumaanishi kitu. Lakini kitu hicho kikubwa kinachonivuta, ndicho ninachojaribu kuelekezea. *Hili* ndilo, loo, naam, vema. Fahamu udogo wako. La tatu . . .

179 Hebu tufikirie. Yeye, kwa mabawa mawili aliyokuwa nayo juu ya uso Wake, Mbele za Mungu, unyenyekevu na . . . ama kicho. Na la pili, Yeye alikuwa na mabawa mawili juu ya miguu Yake. Ilikuwa ni kitu gani? Katika unyenyekevu. Na la tatu, Yeye aliruka kwa hayo, akajitia Mwenyewe katika utendaji. A—akajitia Mwenyewe kazini, kwa mabawa mawili. Huku, mabawa mengine mawili yamefunika uso Wake, katika kicho. mabawa mawili yaliifunika miguu Yake, katika unyenyekevu; na mabawa mawili, Yeye alikuwa kazini. Alikuwa akifanya nini? Alikuwa akimwonyesha huyo nabii. Kwa jambo hili, Yeye alikuwa akimwonyesha nabii jinsi watumishi Wake waliotayarishwa hawana budi kuwa. Huduma iliyoandaliwa na Mungu haina budi kuwa na uchaji, nyenyekevu, na katika matendo.

180 Lakini sasa, kama ukiufunua uso wako, uifunue miguu yako, matendo yako hayatafaa kitu, kwa sababu umechochewa vibaya. Unaona? Inahitaji yote hayo, kukuongoza. Mwenye uchaji, mvumilivu, na katika matendo, hivyo ndivyo Mungu anavyolitaka kundi hili la Kipentekoste kuwa, kwa kuwa Mungu anataka Kanisa Lake liwe kazini.

181 Kama vile yule mwanamke kisimani, mara aliposimama pale na kumwangalia Myahudi huyu aliyekuwa akizungumza naye. Na Yeye akasema, "Mwanamke, nipe maji ninywe."

182 Naye akasema, “Vema, ki—ki—kisima ni kirefu.” Naye akasema, “Huna kitu cha kuchotea. Na jambo lingine, kwanza,” kasema, “hatuna utangamano sisi kwa sisi. Unajua, kuna ubaguzi huku. Vema, hatuna utangamano wowote. Wewe ni . . . Mimi ni mwanamke Msamaria, na—na Wewe ni Myahudi. Hatuna chochote . . . ” Mnaona? Alifuata mwenendo wa kale.

183 Lakini Yeye akamwambia, “Kama ungalijua ni Nani unayesema naye, ama ni Nani anayesema nawe, ungeniomba Mimi maji unywe.”

184 Akasema, “Kisima ni kirefu. Wewe huna kitu cha kuchotea.”

Akasema, “Nenda kamwite mume wako na mje hapa.”

“Mbona,” akasema, “Sina mume.”

185 Yeye akasema, “Umesema kweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.”

Angalieni. Upesi akarudi nyuma. Ilikuwa ni kitu gani?

186 Sio kama wale Mafarisayo. Walipoona hilo likitendwa, wao walisema, “Mtu huyu ni Beelizebuli, mpiga ramli. Ana telepathia ya akili. Mnaona? Hatutahusika . . . Tutalielezea lote vinginevyo, kwa kusanyiko letu. Hata hivyo, Yeye halijui Neno. Sisi tumetoka shuleni. Hatuna kumbukumbu ya Yeye kuja kutoka kwenye seminari zetu.” A-ha.

187 Bali Yeye alikuwa na ile Kweli, Kweli iliyothibitishwa, iliyotolewa na Mungu. Ni jambo gani lililotukia? Mabawa yake upesi yakaufunika uso wake, mabawa yakaifunika miguu yake. Akasema, “Bwana,” sio Beelizebuli. “Bwana, kadiri nijuavyo, hapana shaka Wewe ni nabii. Sasa, ninajua hatujakuwa na nabii kwa mamia ya miaka. Bali Maandiko yanasema, ya kwamba, ‘Ajapo Masihi, Yeye atakuwa ni nabii kama Musa.’ Nasi tunajua, ajapo Masihi, Yeye atafanya mambo haya. Ila sielewi. U nani Wewe? Hapana shaka Wewe ni nabii. Huyu Masihi ajapo, Yeye atafanya jambo lili hili ulilofanya Wewe, kwa kuwa Yeye atakuwa Mungu-Nabii.”

Akasema, “Mimi Ndiye, ninayesema nawe.”

Ndipo akaingia kazini. “Njoni, mwone Mtu!”

188 Yeye alifanya nini leo? Mnasema nini leo hii? “Yeye si wa dhehebu letu,” hakuna uchaji, hakuna unyenyekevu, “kujiunga na makundi yetu.” Wakati wanapoona kanisa likiinuka namna hiyo, “Ni—ni tabaka la kipentekoste. Angalieni mahali lilipotoka, ‘Ndege wa aina moja!’” Hilo ni jema. Hua sikuzote wako pamoja. Kwa hiyo Yeye . . . Vema. Kasema . . . Bila shaka. Wanakula Chakula cha hua pia, sio chakula cha kunguru.

189 Kunguru ni mnafiki. Anaweza kula chakula cha hua, kisha awe mla mizoga, wakati uo huo. Lakini hua hawezi kula chakula cha kunguru. Yeye hana nyongo. Hiyo ni kweli. Akikila, kingemwua. Lakini maskini kunguru anaweza kuketi chini, ale

tunu ya—ya—ya hamu yake mwenyewe ya chakula cha mla mizoga, ashibe, kisha atoke moja kwa moja na kula mahindi pamoja na hua. Lakini, ha-ha, huwezi kufanya hivyo na hua. Yeye anaweza kula tu chakula chake mwenyewe.

190 Naye hua halisi wa Mungu hula Neno pekee. Hawezi kuvichukua vitu vya ulimwengu. La, bwana. Hawezi kuvivumilia. Hivyo tu. Vingemwua. Kwa hiyo kamwe hawezi kuvivumilia.

191 Bali wote waliketi kwenye kijiti kile kile cha kutulia. Kwa hiyo, hapo, jambo ndilo hilo. Walifanya hivyo safinani, nao wamefanya hivyo tangu wakati huo, kwa hiyo haya basi. Yesu alisema, "Yaacheni." Kasema, "Kwenye siku hiyo, ngano itapelekwa ghalani, na kadhalika."

192 Ninawaweka muda mrefu, bali nitaharakisha nikiweza. Angalieni. Upesi tu, simaanishi kulisema kwa ninii yoyote... Mnajua, hili si jambo la mzaha, enyi marafiki. Haya ni Maandiko. Mnaona?

193 Mnyenyekevu, huyo mwanamke akaingia kazini. Kwa nini? Kwanza, yeye alikuwa na kicho. "Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii." Mabawa juu ya miguu yake, juu ya uso wake. Akamtambua. "Wewe ni nabii. Ninaamini hilo. Tunajua ajapo Masihi. Sasa, hatujakuwa na nabii tangu Malaki. Lakini tunafundishwa huku chini, ya kwamba siku moja atainuka mmoja jukwaani, miongoni mwa Wayahudi, na Yeye atakuwa ndiye Masihi. Naye Musa alisema, Yule ambaye tumeambiwa, 'Akiweko mtu miongoni mwenu ambaye ni wa kiroho ama nabii, na yale asemayo mtu huyu yanatimia, basi mnajua hilo.' Hilo ni jambo lile lile tu ambalo Yeremia alimwambia Hanania, na kadhalika, 'Kama hili likitimia, basi tunajua limethibitishwa, ni la kweli.' Na sasa, hapa, Wewe unaniambia ya kwamba nilikuwa na waume watano, na hiyo ni kweli. Nami ninaishi na mwanamume mwingine sasa."

194 "Kwa hiyo ninajua kwamba hapana shaka wewe ni nabii. Ninajua wakati umewadia kwa huyo Masihi kuja, na Yeye atatwambia mambo hayo."

Ndipo akasema, "Mimi Ndiye."

195 Ndipo mara alipojitambulisha Mwenyewe, mwanamke huyo akaingia kazini, moja kwa moja kote mjini, na kusema, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi? Msilikose, enyi watu. Yeye ameketi pale nje juu ya kisiki."

196 Loo, naweza kusema asubuhi ya leo, Masihi yuyo huyo, katika umbo la Roho Mtakatifu, yupo papa hapa sasa, (msilikose, enyi kanisa), akionyesha ishara zile zile na jambo lile lile. "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Ishara zile zile, haina budi kuwa.

197 Kama uhai umo katika mzabibu, unapokua . . . Kama—kama ungeweza kuuhamisha uhai wa mboga katika mzabibu, mbona, utazaa mboga, ama tikitimaji, uhai wowote ulioko ndani yake. Na kama Uzima wa Kristo umehamishiwa ndani yako, na Roho Mtakatifu, unazaa tunda, unaishi yale Maisha.

198 Kwa hiyo, mnaona, kama tunazaa maboga hapa, na tunapaswa kuwa tukizaa zabibu, kuna kasoro fulani. Mnaona? Kwa hiyo, ondoa uhai huo ndani yako. Haikubidi kuuchukua huo.

199 Upaji damu uko wazi, asubuhi ya leo. "Ipo Chemchemi iliyojaa Damu iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli, ambapo wenye dhambi hutumbukia chini ya gharika hiyo." Waigaji wanaweza kutumbukia mle na kupoteza uigaji wao wote, na kupata kitu ambacho ni halisi. Ndipo ushawishi wako utakuwa mkubwa miongoni mwa watu, katika Uwepo wa Mungu.

Huyo mwanamke akaingia kazini.

200 Petro, siku moja yeye alikuwa kidogo katika mashaka, labda. Alimkopesha mtumbwi wake Mtu wa Galilaya ambaye alikuwa wa tabaka la chini sana miongoni mwa watu. Kama Beelizebuli; mpiga ramli; roho mchafu alikuwa juu Yake. "Tunajua ya kwamba Wewe ni Msamaria, na mwendawazimu. Tunajua Wewe una pepo." Nayo makanisa yote yalikuwa yamemtupa nje.

201 Na hata hivyo alikuwa mnyofu kwa Neno ilivyowezekana. Mmoja wenu na athubutu kusema hakuwa hivyo. Hiyo ni kweli. Msiseme Yeye hakuwa hivyo. Alikuwa kinyume kabisa na imani zao zote, bali alikuwa na Neno hasa, angeweza kulithibitisha moja kwa moja katika Maandiko. Kasema, "Ni nani anayeweza kunishtaki Mimi kwamba nina dhambi?" Sasa, Yeye alikuwa nalo.

202 Basi Petro alipomkopesha mtumbwi, Yeye alisema, "Tweka mpaka kilindini, mkashushe kwa ajili ya mvuo wa samaki."

Kasema, "Nilivua usiku kucha. Hakuna kitu mle."

Kasema, "Nilisema, 'Tweka mpaka kilindini.'"

203 "Vema, kama Mtu huyu ndiye Masihi, Yeye ni nabii. Kwa hiyo nitavuta mtumbwi huku." Basi akatupa wavu huko, naye akasema, "Kwa neno Lako, nitauchukua. Maana, sikujui Mimi, bali mazungumzo Yako—Yako—Yako yanasikika ni ya kweli, kwa hiyo nitautupa wavu nione. Basi nikautupa wavu huko." Ndipo wakati ulipozama, yeye alisema, "Ondoka kwangu, Bwana. Mimi ni mtu mwenye dhambi."

204 Jambo lile lile ambalo ilimbidi Isaya kusema, "Ondoka kwangu. Bwana, mimi ni mtu mwenye midomo michafu. Ninaishi miongoni mwa watu wachafu." Alikuta kwamba Neno la Mungu lilifanya kazi, ukimwamini Mungu katika Neno Lake.

205 Yule kipofu, alipoponywa, asingeweza kutulia. Kwa nini? Alikuwa ameingia kazini. Petro aliingia kazini. Yule mwanamke

aliingia kazini. Yule kipofu, asingeweza kutulia. Yeye alisema, "Mtu huyu ni . . . "

"Mpe Mungu utukufu. Tunajua mtu huyu ni mwenye dhambi."

206 Kasema, "Ni jambo la ajabu kwamba ninyi nyote hamjui Yeye ni Nani, na mkiwa viongozi. Ni jambo la ajabu ile siku imetufikia, kwamba Mtu angeweza kuyafungua macho ya kipofu, nanyi makasisi hamjui kwamba Yeye ni Nani." Mtu huyo alikuwa na theolojia nzuri.

207 Kasema, "Hiyo ni ajabu, miongoni mwenu watu mnaodhaniwa kuwa viongozi wa kiroho wa siku hizi. Nayo macho ya mtu yamefunguliwa hapa; mimi nikiwa kipofu. Mnajua mimi ni kipofu. Mnajua nilikuwa kipofu, na sasa ninaweza kuona." Kasema, "Kwamba Yeye ni mwenye dhambi, ama siye, sijui mimi. Bali ninajua jambo moja: ninaweza kuona; ambapo, nilikuwa kipofu, hapo kabla."

208 Akaingia kazini. Alikuwa ameufunika uso wake, akaifunika miguu yake. Akasema, "Bwana, ni Nani huyu, nipate kumsujudu?" Ndipo alitaka kujua. Yule kipofu, hakika, yeye alieneza sifa Zake kote, kila mahali.

209 Sikilizeni. Wale watu kwenye Pentekoste, waliifunika miguu yao. Walizifunika nyuso zao. Hawakujali yale Wayahudi waliyosema. Walikuwa na agizo kutoka kwa Mungu, Neno la Mungu, kwenda hekaluni, hadi Yerusalemu, na kungojea huko Yerusalemu mpaka Roho Mtakatifu atakapokuja. Nao hao hapo, wakilitii Neno Lake. Unyenyekevu; kusujudia.

210 Wakati, kanisa lilikuwa likiwacheka. "Kundi la waasi liko kwenye chumba cha juu huko juu."

211 Nyuso zimefunikwa, Uweponi mwa Mungu! "Loo, Bwana, Wewe ulitoa ahadi. Kukiwako na uovu wowote ndani yangu, nisafishe, Bwana." Mara yakaja mabawa ya kutenda kazi, nao wakaingia kazini. Hao waliokuwa wameogopa, wasingeweza kutoa ushuhuda mtaani. Walikuwa mtaani, wakinena kwa lugha zingine, na—na wakiwa kazini.

Kiasi kwamba watu walisema, "Watu hawa wamelewa kwa mvinyo mpya."

212 Ndipo Petro, yule ambaye angeyaweka Maandiko, kuyanyosha Maandiko, akasema, "Watu hawa hawajalewa kwa mvinyo mpya. Bali *hili* ni Lile."

213 Nami daima nimesema, "Iwapo *hili* silo *lile*, nitaliweka tu *hili* mpaka *lile* litakapokuja." Kwa hiyo na—napenda *hili* sana, nitakaa tu na *hili* mpaka Lile litakapofika hapa. Ninaamini *hili* ndilo Lile. Vema. Vema. Naam.

Waliiona ahadi ya Mungu imetimizwa. Ikawaweka katika matendo.

214 Basi yale tumeona, yale tumeona, ahadi Zake katika siku hizi za mwisho, yale tumeona, sisi wenyewe, yanapaswa kumwingiza kila mmoja wetu kazini.

215 Lakini mnajua ni kwa nini? Hatuzifuniki nyuso zetu na miguu yetu vizuri. Mabawa yetu hayatafanya kazi. Mnaona? Tumeyapanua mabawa *haya*, na kuyapanua mabawa *haya*, na tunajaribu kuyapanua *haya*, pia. Tunapulizia tu hewa. Mnaona? Jifunike, jinyenyekeze, kisha uingie kazini. Loo, jamani!

216 Yale tumeona yakitendeka yanapaswa kumweka kila mtu kazini. Linapaswa kufanya kanisa ambalo lingeanzisha uamsho hapa Phoenix, hata watu wangekuwa wakiruka kuja huku kutoka Ulaya, kuona yale yanayotendeka. Wangesema, "Kuna mahali huko Arizona panapoitwa Bonde la Maricopa, mji unaoitwa Phoenix. Kuna kitu kilichotokea kule hata zile ngurumo saba za Ufunuo 10, ambazo hata hazijaandikwa katika Biblia, zinadhihirishwa."

217 Nguvu za Mungu, wakati wa mwisho upo hapa. Malaika amezikusanya zile sehemu legevu nasi tupo hapa. Amina. "Yeye alikuwa tayari kuziandika ngurumo hizo, ndipo Yeye akasema, 'Usiziandike. Zitie muhuri.'" "Basi katika siku hiyo ya kutoa sauti ya malaika huyu wa mwisho, wa saba," wakati wa saba wa kanisa, wakati wa kanisa la Laodikia, "siri ya Mungu," yote kumhusu Mungu, jinsi ambavyo Mungu si lundo kubwa la miungu, bali ni Mungu mmoja, "na mambo haya mengine yote yanapaswa kutimizwa yote katika wakati huo."

218 Vile vita vikuu, huko nyuma awali, viliacha sehemu legevu zimening'inia nje. Zote zinapaswa kukusanywa pamoja, katika wakati huu wa mwisho. Kasema, "Basi hiyo itakapotoa sauti yake, Malaika atashuka chini na kusema, 'Hapatakuwa na wakati baada ya haya. Nitaapa kwa Yeye aliye hai milele na milele, hapatakuwa na wakati baada ya haya.'"

219 Loo, tupo hapa, ndugu, dada. Tuko kwenye wakati huo. Hebu tumwache Roho Mtakatifu atushawishi kwenye Neno la Mungu. Hebu tumwache Mungu aishawishi mioyo yetu, na tusishawishiwe na wengine. Mnaona? Hili linapaswa kutuweka kazini kwa uchaji na unyenyekevu, ile Nguzo ya Moto ikithibitishwa miongoni mwetu tena, kama ilivyokuwa, ikiwaleta wana wa Israeli. Ishara za Kuja Kwake zimewadia. Loo, jamani! Neno, kwa Neno likitimizwa, tunaiona ile ahadi, "Siku za mwisho, Yeye angeimwaga Roho Yake."

220 Watazame Wapresbiteri, Wamethodisti, na Wabaptisti. Wanaingia kwenye mwenendo huu. Mlijua hilo? Sikilizeni, ndugu. Hivi hamyaelewi Maandiko? Biblia ilisema, "Hapo wanawali waliolala walipokuja kununua Mafuta, huo ndio wakati ambapo Bwana-arusi alikuja."

221 Nimeona katika Wafanyabiashara wenu wa Full Gospel, jinsi mnavyoingiza akina "Father *Nanii*," Mpresbiteri; mnaingiza

"Father *Nanii*," Mkatoliki, na wote hawa. Jambo lingine, hao si "Baba." Biblia ilisema, "Usimwite mtu yeyote Baba humu duniani." Wao ni wahudumu. Nami ninawaheshimu kwa heshima yoyote wanayoweza kuheshimiwa, bali hampaswi kuwaita "Baba."

222 Na, ninyi Wafanyabiashara, ninatumaini mhariri huyo yupo hapa asubuhi ya leo. Naam. Inakuwaje mnaandika azimio huko nyuma, ya kile kanuni zenu za imani zilicho, na vitu kama hivyo, na muwe wa baina ya madhehebu? Heri mtoke kwenye jambo hilo. A-ha. Vema.

223 Angalieni, ndugu zangu. Sikilizeni. Bwana-arusi alipokuja, mwanamwali aliyelala aliamka. Kisha sa—sauti ikaja, "Tazama, Bwana-arusi yuaja." Hiyo ndiyo siku tunayoishi?

Ndipo mwanamwali aliyelala akaamka, Wamethodisti, na Mpresbiteri, Katoliki, na wote, wakaingia, "Loo, tupeni kidogo, Mafuta haya. Tunaliona."

224 Wao wakasema, "Tunayo tu ya kututosha sasa. Inawabidi kuyakeshea, ninyi wenyewe." Ndipo walipokuwa wakikesha, Bibi-arusi akaja.

225 Na kamwe katika historia ya wakati wa kanisa, kamwe katika historia ya milki ya kipentekoste katika miaka hii hamsini iliyopita, hakujawa na wakati ambapo ulimwengu wa kimadhehebu unaingia kwa fujo jinsi unavyofanya sasa. Hivi hamtambui ya kwamba huu ndio wito wa mwisho? Na, hata hivyo, tunaendelea tu kiholela kana kwamba hata hakuna kitu kinachotendeka. "Utukufu kwa Mungu! Ninaweza kucheza katika roho. Ni . . . " Loo, loo, loo, loo! Jamani!

226 Yesu alisema, "Wengi watakuja Kwangu siku hiyo, waseme, 'Bwana, Bwana, sikufanya mambo haya?'" Unyofu! Ushawishi wako! Jamani! Naam.

227 Yale tumeona yakitukia yanapaswa kututia kazini. Sisi, kama vile nabii Isaya, tumeona madhehebu yanayojitukuza yakipoteza mahali pao.

228 Kulifanyika nini wakati uamsho ulipokuja pamoja na Luther? Wao walifanya nini? Kitambo kidogo tu, nao wakajiundia dhehebu, wakaliunda dhehebu la Kilutheri; wakachora mstari mdogo, kasema, "Sisi ni Walutheri. Wengine wenu mko nje." Mungu akalivunjilia mbali, kwa John Wesley.

229 Ndipo John Wesley alipoondoka; Charles, na John, na Asbury, na kwa hivyo, walipoondoka jukwaani, hao waliliundia dhehebu. Mlifanya nini? Mlichora mstari ule ule kama kanisa Katoliki liliochora, mkaunda dhehebu.

230 Kamwe hapakuwapo na dhehebu mpaka kanisa Katoliki. Ndiye mama wa wote hao. Sasa, ninyi mnaoijua historia, mnajua hiyo ni kweli, lile Baraza la Nikea.

231 Sasa, tunaona, kwamba hapo ninyi mlijiundia dhehebu. Mlifanya nini? Lilikufa. Wamethodisti walikufa papo hapo. Kamwe halijasonga, tangu.

232 Wakaja Wapentekoste, nanyi mkafanya nini? Lile Assembly Kuu, linalojulikana kama Assemblies of God, loo, mlijiundia dhehebu. Mlifanya nini? Mkaanza kuoza.

233 Ndipo likaja la Umoja, lilivyoitwa, "Hoja Mpya." Mkafanya nini? Mkaondoka mkajiundia dhehebu. Mungu akaongeza kitu kidogo kanisani, nanyi, "Loo, tumelipata, nanyi nyote mko nje ya Hilo." Loo, jamani, ndugu! Huyo si Mungu. Hivi hamwoni? Mlifanya nini? Mkafa papo hapo njiani.

234 Mungu akawainua Wafanyabiashara Wakristo, hapa katika siku za mwisho. Na kama wakianzisha jambo lile lile, watakufia papo hapo. Hiyo ni kweli kabisa. Kamwe msifanye hivyo.

235 Kitu gani? Ni kitu gani kilichotukia? Isaya aliona mtu mashuhuri akipoteza ushawishi wake na kufa.

236 Na vivyo hivyo sisi tumeona wakati, katika siku hizi za mwisho, ambapo, Mungu, Yeye, si lazima amwinue Mpentekoste. Yeye anaweza kumwinua Mpresbiteri, Mbaptisti. Anaweza kumwinua mtu asiyetoka kwenye yoyote ya hayo. Kweli. "Yeye anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto."

237 Nasi tunamwona akitoka moja kwa moja nje ya matabaka ya Kipentekoste, na kumwinua mtu asiyejua lolote kuwahusu, awafanye—awafanye kujionea aibu. Kisha mnamkataa, mnasema, "Loo, upuuzi! Mbona, mzee wa jimbo angenifukuza papo hapo." Loo, ndugu! Mnaona mahali mmefikia? Isaya aliliona hilo likipoteza milki yake, nasi tunayaona madhehebu hayo yakipoteza milki yao.

238 Loo, ninyi mna idadi kubwa. Hiyo ni kweli. Ni heri nyinyi. . .Mungu alisema, "Ulipokuwa mdogo, uliniheshimu. Na—nami. . .Ulipokuwa mdogo, ningeweza kuzungumza nawe. Lakini ulipokuwa mkubwa sana, nisingweza kuzungumza nawe, ndipo ilikubidi kwenda peke yako."

239 Hivyo ndivyo tunavyofanya, kama mtambo mkubwa mno, Duesenberger ya silinda kumi na sita. Tunao mtambo wa kisiasa na—na mtambo katika—katika hii mienendo. Ni wazee wa jimbo na—na mambo haya mengine yote yanayokidhibiti kitu hicho, naye Roho Mtakatifu amehesabiwa nje. Ukijaribu kufanya kitu ambacho ni kinyume kidogo na fundisho lako, wao wanasema, "Ai, upuuzi!" Lichunguze kwa Neno. Ni Neno, liamini; kama sivyo, achana nalo. Mungu atalithibitisha Neno Lake. Kweli.

240 Sasa, Uzia aliona kwamba mtu huyo. . .Ninaenda kusema jambo fulani. Na mimi sitaki kuudhi, bali nataka kulifanya lishike. Uzia. . .Yeye alimwona mtu mwenye ushawishi mkubwa (nini?) akipoteza milki yake, kwa sababu alikosa kulitii Neno.

Hiyo ni kweli? Sasa, tumeishi kuiona siku ile ile, ambapo madhehebu haya yote makubwa yanapoteza ushawishi wao. Mungu anaiendea sehemu nyingine mahali fulani, anachukua kitu ambacho hakihusiki nanyi. Mnaona? Tumeliona.

241 Madhehebu haya makubwa, kwa kanuni zao za imani, yanapoteza milki yao. Kwa nini? Wanajaribu kujitengenezea kitu fulani kupachukua mahali pa ofisi yake aliyetiwa mafuta. Whiu! Mnajua hiyo ni Kweli. Kamwe hamtaweza kufanya jambo hilo. Mungu atamchukua mtiwa mafuta Wake, nawe huwezi kuiga ofisi hiyo. Mungu hutia mafuta. Yeye humchagua yule Yeye amtakaye. Humhukumu yule Yeye atakaye. Mungu ndiye anayehesabia haki. Mungu ndiye huchagua, na Yeye humwinua. Ndipo tunalikataa, na kisha tunaona ushawishi umepotea. Mungu anasonga mbele moja kwa moja, katika unyenyekevu Wake, katika njia Yake ya unyenyekevu; na kulitoa kundi moja kwa moja, kwa ajili ya Jina Lake, kama Yeye alivyoahidi angefanya. Naam.

242 Sisi, kama Uzia, tunayaona madhehebu makubwa yakipoteza mahali pao, kwa sababu wanajaribu kuchukua mahali pa aliyetiwa mafuta, pamoja na dhehebu, badala ya kulichukua Neno lililotiwa mafuta.

243 Uzia alikuwa ni mfalme mkuu. Mungu alimfanya mfalme. Hilo ni sawa. Bali alipojaribu kuchukua, mwenyewe, na kujifanya kuhani, asingeweza kufanya hivyo.

244 Hatuwezi kujifanya chochote. Huwezi kufanya maaskofu, na manabii, na kadhalika. Huwezi kujitengenezea hilo. Halina budi kuzaliwa ndani yako. Halina budi kuwa ni Roho wa Mungu, kuchaguliwa tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu. "Mungu aliweka kanisani." Mungu alifanya yale aliyofanya. Na tunapojaribu kuiga, tunapoteza ushawishi wetu. Loo, enyi kanisa! Kwa nini hatuwezi . . .

245 Sikilizeni. Ni kama mchezo wa mpira, mtu fulani kwenye mchezo wa kandanda. Mtu fulani anaupata mpira, na kila mmoja wa wachezaji wake anajaribu kumnyang'anya mpira. Hamwezi kushinda huo mchezo.

246 Kuwa mlinzi, ulinde huo mpira, sio kujaribu kumnyang'anya mwenzako.

247 "Utukufu kwa Mungu! Kama anaweza kufanya hivyo hapa kwenye kona *hii*, Mungu ambariki."

248 "Mimi—mimi—mimi ni wa Umoja, ninaweza kufanya hivyo." "Mimi ni wa Utatu, ninaweza kulifanya." "Hana shughuli yoyote kufanya hivyo." Unapiga mpira kutoka mikononi mwa wachezaji wako mwenyewe.

249 Nyinyi nyote Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, Walutheri, umoja, uwili, utatu, kama unaendesha ngamia wa kinundu kimoja, ngamia wa vinundu viwili, ama kama

una vinundu dazani moja, inaleta tofauti gani? Hebu sote tuje kwenye chemchemi hii, "Chemchemi iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli, ambamo wenye dhambi hutumbukia chini ya gharika hiyo."

250 Hebu tuulinde Mpira. *Huu* ndio Mpira. Roho Mtakatifu anajaribu kuubeba. Atauhukumu ukomunisti. Ataihukumu dhambi. Atauhukumu uovu. Atamdhihirisha na kumtukuza Yesu Kristo, na kuuleta Utu Wake miongoni mwa watu. Amina. Hakika. La. Naam, bwana.

251 Lile ono la nabii lilisababisha maungamo. Hebu ingia tu katika Uwepo wa Mungu, wakati mmoja. Ukiona ono, ono la kweli kutoka kwa Mungu, utaona jinsi ulivyo mdogo. Hiyo ndiyo sababu niko kwenye Pwani ya Magharibi sasa. Tazama. Ingia tu katika Uwepo wa Mungu, wakati mmoja, uone linalotukia. Mnaona? Lilimfanya nabii . . . Nabii huyu alifanyaje?

252 Kweli nitafunga. Huyo nabii, mtu mwenye ushawishi, mtu aliyeitwa; zaidi ya askofu, zaidi ya mzee wa jimbo, zaidi ya kasisi, digrii ya udaktari. Yeye alisema, "Mimi ni mwenye dhambi, nami ni mtu mwenye midomo michafu." Whiu! Mtu aliyekuwa na wadhifa kama nabii, na, wakati hao Malaika walipokuja kule, naye akatambua kwamba alikuwa ni mwenye dhambi.

253 Na hata hivyo wanawake wetu wanaweza kuwa na nywele fupi, kucheza katika Roho. "Mvua huwanyeshea wenye haki na wasio haki."

254 Wanaume wetu wanaweza kushikilia madhehebu yao, na kuita kila kitu kingine ibilisi, kisichokuwa pamoja nao; na wangali watacheza katika Roho, na kuhubiri Injili, na kujiita wenyewe . . . Loo, ndugu, kuna kasoro fulani. Hiyo ni kweli.

255 Sasa, msi—msinikasirikie. Aminini. Iweni—iweni—iweni tu waaminifu mbele za Mungu, ninapomalizia hapa, dakika moja.

256 Ilimfanya nabii huyu mkuu kusema, "Mimi ni mwenye dhambi. Mimi, mimi ni mtu mwenye midomo michafu." Ndipo, alipokuwa tayari kuungama, ndipo ukaja utakaso. Mliona jambo hilo? Yeye alisema, "Loo, mimi ni mtu aliyepotea. Mimi ni mtu mwenye midomo michafu, ingawa mimi nina cheo cha juu kuliko wote wa kiroho, ama wadhifa wa kiroho, nchini. Mimi ni nabii wa nchi hii, bali ni mchafu. Midomo yangu si safi. Nimepotea kabisa. Ole wangu. Namwona Bwana Mungu wa majeshi."

257 Wakati hao Malaika walipokuwa wamezifunika nyuso Zao, wapate kusimama Uweponi Mwake, ndipo unatambua. Laiti kanisa lingalitambua tu ya kwamba huyu Roho Mtakatifu ndiye Bwana Mungu wa majeshi! Zifunikeni nyuso zenu, miguu yenu. Shukeni.

258 Yeye aliungama, angalieni, ndipo ukaja utakaso wake. Sasa nitasema jambo fulani, bali msiudhike. Utakaso wake kamwe

haukuja kwa kanuni za imani. Ulikuja kwa Moto. Utakaso wake haukuja kwa azimio la kitabu fulani, yale *Fulani-wa-fulani* aliyosema. Utakaso wake ulikuja kwa Moto. Yule Malaika alienda akatwaa Moto kutoka madhabahuni na kuuweka juu ya midomo ya nabii. Utakaso huja kwa njia ya Roho Mtakatifu na Moto, sio shahada mpya ya sanaa, ama digrii ya udaktari, ama kitu fulani.

259 Kama vile Parris Reidhead alivyosema sio muda mrefu uliopita, wakati alipompokea Roho Mtakatifu, kwenye chumba changu cha mbele, yeye alisema, "Ndugu Branham, ninazo digrii za kutosha kuukandika ukuta wako. Bali Mungu yuko wapi katika hizo zote?" Alisema, "Je, hao walimu wamekuwa makosani?"

260 Nikasema, "Ati mimi, nikiwa na elimu ya darasa la saba, niseme hao walimu wamekosea? Si mimi. Walikuwa sahihi katika yale waliyofundisha, nadhani, bali hawakufundisha kwa kilindi vya kutosha."

261 Kama vile yule mtu aliyekuwa akila tikitimaji, yeye alisema, "Sehemu hiyo ilikuwa nzuri, lakini kuna zingine zilizosalia?" Ati umpe tu aonje, halafu umnyang'anye? La, bwana.

262 Kama vile kumlisha ndege kurumbizi, vipande vikubwa mno vya vitamini, kufanya mabawa makubwa mno ya madoadoa, na kwa mabawa, na kufanya mifupa mizuri, na kumfanya ndege mkubwa mwenye nguvu, halafu umweke katika kizimba. Hawezi kuyatumia.

263 Mwachilie. Acha Mungu aanze kumfanyia kazi, amwingize kazini, kama yuko tayari kuifunika miguu yake. Hiyo ni kweli. Lakini sasa, kumbukeni, halitafanya kazi mpaka uifunike miguu yako.

264 Utasimama tu, upunge upepo, "Mimi ni Assembly. Mimi ni Umoja. Mimi ni *hili*." Unasimama tu pale, ukipunga upepo, huendi popote.

265 Lakini mara ukiufunika uso wako, uifunike miguu yako, halafu uingie katika matendo. "Bwana Mungu, mimi hapa."

266 Kwanza huja utakaso. Angalia. Na baada ya utakaso kulikuwako na agizo. Loo, jamani! Naam. Kwanza ni kuungama, kisha utakaso, na halafu agizo. Mbona, baada ya Isaya aliyetakaswa kutakaswa kwa Moto, ndipo yeye akalia akiisha kutakaswa, "Bwana, mimi hapa. Nitume mimi."

267 Loo, enyi kanisa, wafanyabiashara, hebu tusipoteze ushawishi wetu. (Ninafunga.) Hebu tuzifunike nyuso zetu asubuhi ya leo. "Bwana, mimi si kitu. Bwana, nifinyange na kunifanya upya. Niko huku chini hekaluni. Jalia niifunike miguu yangu. Bwana, si kitu mimi. Niko tayari kuyasahau yote niliyowahi kujua. Kama vile Paulo, 'Sijui chochote, ila Kristo, na Yeye amesulubishwa.' Nijalie, Bwana, nijinyenyekeze."

268 Ndipo basi unaposimama kutoka hapo, pamoja na maungamo halisi, utakaso halisi, ndipo wito utakapokuja, "Ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?" basi, Isaya, unaweza kujibu, "Mimi hapa. Nitume mimi." Maisha yako yataishawishi familia yako. Yatamshawishi jirani yako. Yatalishawishi kanisa lako. Yata . . .

269 Hebu weka mfuasi mmoja ama wawili wazuri kanisani, ambao kweli wanawaka moto kwa ajili ya Mungu, italifanyia kanisa hilo jambo fulani, kuliko miamsho arobaini mngaliweza kuwa nayo. Kweli. Mfuasi mzuri, aliyetakaswa, ataweka mfano, huku akiwa na uso unaonawiri kwa utukufu wa Mungu, pamoja na utamu na unyenyekevu, kusimama hapo katika nguvu za Mungu. Basi, angalia, mtu anapokuwa ni mgonjwa, watamwita mtu huyo aje aombe. Ama, huenda mkawadhihaki, na tairi lao limetoka pumzi, na kadhalika. Huenda upuuzi huu wote mkausema. Lakini hebu mauti yakupige wakati mmoja, utakuja kujua, wakati hayo mapambano yanapoanza kuja, ni nani mtu huyo aliye mwaminifu kweli kanisani.

270 "Mimi hapa, Bwana. Nitume mimi. Jalia ushawishi wangu uwe juu ya wengine, Bwana. 'Kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida.' Jalia Neno hili linishawishi. Na maombi yangu ni, Bwana, wakati nikiwa kwenye bonde hili hapa, la Bonde la Maricopa, maskini sehemu ndogo ya jua ulimwenguni, jalia niwe na mawasiliano na Mwana wa Mungu, hiyo ingeutawanya mwangaza wa jua la Roho Mtakatifu kote humu bondeni. Na itawafanya ndugu, na wanawake, na akina dada, na hata wenye dhambi, kupata chemchemi hii iliyojaa Damu."

271 Jalia sisi sote tuje kwenye mahali pa hekalu, ambapo tunaweza kujitambua wenyewe wachafu, na kuishi maisha ambayo yatawashawishi wengine kumpenda Kristo.

Na tuombe.

272 Wakati tumeinamisha vichwa vyetu, nitavumisha. Ninii sana . . . Siwezi kuimba. Ninyi nyote uvumisheni tu pamoja nami, nikiyasema hayo maneno.

> Wakati kaa la Moto lilipokuwa limemgusa nabii,
> Likimfanya kuwa safi iwezekanavyo,
> Wakati sauti ya Mungu iliposema, "Ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?"
> Ndipo akajibu, "Bwana, hapa, nitume mimi."
>
> Nena, Bwana wangu.

Sote pamoja, sasa.

> Nena, Bwana wangu,
> Nena, nami nitakuwa mwepesi kukujibu;
> Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
> Nena, nami nitajibu, "Bwana, nitume mimi."

Kwa uaminifu sasa, sikilizeni:

Mamilioni sasa wanakufa katika dhambi na aibu;
Kisikieni kilio chao cha huzuni na uchungu;
Hima, ndugu, hima ukawaokoe;
Upesi jibu, "Bwana, mimi hapa."

Wote wanaotaka kwenda, inueni mikono yenu sasa.

Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
Nena, nami nitakuwa mwepesi kukujibu;
Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
Nena, nami nitajibu, "Bwana, nitume mimi."

273 Baba wa Mbinguni, jalia hilo liwe kilindi cha moyo wetu, Bwana. Kwa kweli mamilioni sasa wanakufa katika dhambi na aibu. Mumu humu katika jiji la Phoenix, maelfu hasa wanapapasa-papasa dhambini. Nasi hapa tumesimama, asubuhi ya leo, tumefunikwa kabisa na Uwepo wa Roho Mtakatifu. Sote tunautambua Uwepo Wake adhimu. Ninamhisi moyoni mwangu. Ninamhisi juu ya watu.

274 Ee Mungu, jalia ono litujie, tupate kuuona utakatifu wa Mungu, tuone jinsi tulivyo wadogo. Jalia nguzo za hekalu zitikisike mbele zetu, na hapo wakati tukiwa katika Uwepo Wake, Bwana. Jalia nguvu za Roho Mtakatifu zitutikise sana, Bwana, ili kwamba si nguzo za hekalu tu zitakazotikisika, bali nguzo zilizomo mioyoni mwetu zitatikisika, nguzo ya kutokujali, itakayofanya mlango wa nafasi ya Mungu kuingia. Liondolewe, jiwe la kutokuamini liondolewe.

275 Na tujalie, Bwana, tujibu upesi, "Bwana, ninajinyenyekeza. Ninataka mabawa juu ya miguu yangu, juu ya uso wangu." Kwanza, Bwana, ninyenyekeze, nipate kuwa ushawishi kwa wengine. Tujalie, Bwana.

276 Ubariki mkutano huu mkubwa. Ibariki mikutano hii inayokuja. Na makanisa haya, hawa, ndugu zangu, Bwana, mbele ya upinzani, wameniita na kuniomba nije huku chini, nikazungumze katika makanisa yao. Ee Mungu, washa kila mshumaa. Tujalie, Bwana. Jalia kuje Nuru kuu sana, uamsho mkuu sana kote katika Phoenix. Tujalie, Bwana, kwamba hili litafanyika miongoni mwa makanisa yote, na watu Wako wote, katika mahali pote, katika madhehebu yote.

277 Na wengi wa hao watu wa thamani huku nje mtaani wanatazama, na kushangaa, na kungojea kuuona Uzima wa Kristo ukidhihirishwa miongoni mwa watu Wake. Tujalie, Bwana.

278 Huenda tusiweze kulishawishi jiji lote. Hilo halijapata kutendwa, kwa maana humo ndani ngano na magugu yako pamoja. Lakini, Bwana, jalia tuchochewe sana, hata tutajaribu kuwasha mshumaa mmoja mdogo kila siku, kwa kumwambia

mtu mwingine, kufanya jambo fulani litakalowashawishi wengine kukujua Wewe na kukupenda, kwa kuwa kukujua Wewe ni Uzima. Tunaomba baraka hii.

279 Mbariki Ndugu yetu Williams hapa, Bwana, na Dada Williams. Tunawapenda. Wao, wao ni—wao ni watumishi Wako. Tunaamini katika unyenyekevu, Bwana. Wao wanasujudia miguuni Pako. Tunashukuru sana kuona jinsi unavyotenda kazi miongoni mwa familia yao, na pamoja na binti zao—zao na mwa—mwana wao. Na jinsi ulivyowarehemia!

280 Ndugu Rose, na wengi sana wa hao wengine hapa, Bwana, wa wanaume, wa wanaume mashuhuri; na ndugu zangu wahudumu walio kote mjini; na dada zangu, Bwana, ambapo ndio... Hao ni watoto Wako. Na mimi—mimi ninataka kuweka bega langu pamoja nao—pamoja nao, Bwana. Ninataka kusukuma kwa nguvu. Nisaidie, Ee Mungu. Mimi ni mdogo. Mimi ni mdogo, wala siwezi kusukuma kwa nguvu sana. Bwana, jalia nisimame pale, na Wewe usukume. Tujalie, Bwana, kwamba tuweze kuusogeza mzigo huu mkubwa wa Mungu, kwenye Ufalme wa Mungu. Tujalie, Baba.

281 Tunalikabidhi hili lote Kwako, sasa, tunapoenda mbele tangu leo. Nasi tunajikabidhi wenyewe, na tunaomba kwa ajili ya uamsho mkuu. Pia jalia Wafanyabiashara Wakristo waweze kuchukua kutoka hapo na kuendelea moja kwa moja. Na jalia, mara tu wao...huu mkutano mkubwa utakapokwisha, jalia makanisa yote yashike moto, nao uamsho ukiendelea mbele na zaidi na zaidi. Jalia tuweze kuuanzisha huo moto, Bwana. Pia jalia Roho Mtakatifu apulizie miale hiyo, mpaka jumuiya yote huku inawaka kwa moto wa kipentekoste. Tujalie, Bwana. Tunayakabidhi yote Kwako, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana Wako. Amina.

282 Samahani kwa kuwaweka muda mrefu sana, kwa sababu sasa ni karibu adhuhuri. Hata tunaweza kungojea chakula cha kutwa, nadhani. Na kwa hiyo, lakini, ni—ninashukuru kuwa hapa. Ushirika wenu, ushirikiano wenu umekuwa mwingi.

283 Nanyi ndugu zangu, ni wangapi hapa ambao nitakuwa makanisani mwenu juma hili? Inueni mikono yenu kote. Hilo ni sawa. Ndugu na dada, hapa karibu, asanteni. Nasi sote tunawaalika huku, juma hili, mikutanoni.

284 Sasa nitamwachia Ndugu Williams hapa sasa, kwa ajili ya kufunga. [Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu Williams anasema, "Yeye anaweza kufanya kazi hii vizuri kuliko niwezavyo."—Mh.] Vema.

Inamisha kichwa chako kwa dakika moja tu basi.

285 Ni wangapi wanaotaka chini madhabahuni asubuhi ya leo, unataka kweli wito wa madhabahuni moyoni mwako? Utainua mkono wako? Useme, "Mungu, nifanye kile ninachopaswa kuwa.

Mimi, mimi ni udongo. Wewe ni Mfinyanzi." Mungu akubariki. Mungu akubariki.

286 Sasa, mnapoiweka mikono yenu chini, kuna mtu fulani hapa ambaye kamwe hajamkubali Kristo, hajui maana yake? Huenda ukawa. . . Unaninii tu, loo, labda chini ya ushawishi fulani ambao kamwe haukukusaidia hata kidogo. Mara tu hicho kitu, kama ushawishi, kilipoondoka, kipindi kidogo cha mhemko, bali uliendelea kuishi maisha yale yale.

287 Ama labda kamwe hujawahi kumkubali Yeye, hata kidogo, nawe ungetaka kusema, asubuhi ya leo, "Mungu, jalia Neno hilo lizame ndani yangu mpaka ninaweza kuufunika uso wangu katika unyenyekevu, na kuifunika miguu yangu, na kupiga magoti madhabahuni Pako, mpaka wa—wale Makerubi wataupeperusha utukufu wa Mungu juu ya nafsi yangu, na kunisafisha kwa Moto Wake mtakatifu." Waweza kuinua mkono wako, useme, "Ndugu Branham, niombee. Nipo hapa nikihitaji maombi?" Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Loo, Mungu akubariki. Kwamba, ukiinua mkono wako, unafanya uamuzi moyoni mwako. Mungu akubariki, ndugu yangu.

288 Mtu mwingine, baadhi ya dada zetu hapa inua mkono wako, useme, "Ndugu Branham, siamini kwamba ndivyo ilivyo, kwamba wewe ni. . . kwamba unasema. Wanakuita mchukia wanawake. Siamini hilo. Ninaamini unanipenda, kama dada yako." Nami nakupenda, dada. Lakini ninajaribu tu kukwambia. Sitaki ushawishiwe na Marilyn Monroe. Ninataka wewe ushawishiwe na Yesu Kristo, unaona, na Neno Lake. Yeye ni Neno. Iwapo Neno halikushawishi, basi Kristo hawezi, kwa sababu Yeye ni Neno. Mnajua hilo.

289 Niliota ndoto sio muda mrefu uliopita, ama ono, hasa. Haikuwa ndoto. Nilikuwa nimesimama pale pale. Nilikuwa huko nje mwituni, kwenye doria. Nami nikawaona wanawake wawili. Na mmoja wao alikuwa . . . Kanisa moja la Kipentekoste lililiandika, na lingine huyo mwingine. Ndipo nikasema, mmoja akasema, "Dada, unafikiri ni sawa kwa Ndugu Branham kutukemea sana namna hiyo?" Kasema, "Kama Yesu angalikuwa hapa," kasema, "Labda asingelisema."

290 Nao hawakujua nilikuwa ni nani, nami nilikuwa nimesimama pale. Nikasema, "Vema, sasa, sikilizeni. Mtu huyo hapana shaka anasema kweli. Haijalishi, kama hujawahi kumwona Yesu, ndivyo ama sivyo, kama Yeye yupo hapa, Yeye hawezi kubadilisha Neno Lake. Litakuwa ni vile vile tu."

Wakasema, "Vema, hiyo ni kweli kabisa, sivyo?"

291 Loo, huwezi kuona ni kweli, ndugu, dada? Huwezi kuona kwamba Kristo hawezi kubadilisha Neno Lake? Yeye ni Neno.

292 Huenda kuna wengine zaidi? Inua mkono wako, useme, "Nikumbuke, Ndugu Branham. Ninajua mimi siko sawa.

Niombee sasa." Unaweza kuinua tu mkono wako? Mungu akubariki. Wewe maanisha hilo. Ubarikiwe. Ubarikiwe. Hilo ni jema. Hilo ni zuri. Mungu akubariki. Limaanishe tu kabisa, kutoka moyoni mwako. Tunafikia mwisho wa safari sasa, muda kidogo tu zaidi.

293 Labda kwenye ule mkutano, usiku nitakaozungumza; nami nina usiku, usiku mmoja, angalau, kwenye ule mkutano. Ninataka kuzungumza juu ya baadhi ya mambo hayo, jambo tu kutoka moyoni mwangu, na sababu yenyewe ya mimi kusimama hapa asubuhi ya leo. Kunao watu papa hapa ndani wanaoweza kusema, "Amina, na Amina," sababu ya mimi kusimama hapa asubuhi ya leo. Jambo fulani limetukia ambalo halijawahi kutukia hapo kabla maishani mwangu. Hiyo ni kweli. Limetukia tu, nalo likaniita mumu humu Arizona. Nipo hapa kwa ajili ya jambo fulani.

> Mamilioni sasa wanakufa katika dhambi na aibu;
> Sikilizeni tu kilio chao cha huzuni na uchungu.

294 Ni kitu gani kinachowafanya watu wafanye makosa? Ni kiu ndani yao. Mungu aliwafanya kuona kiu, mnaona, kumwonea Yeye kiu. Nao wanajaribu kuridhisha huo—huo wito mtakatifu kwa mambo ya ulimwengu, kujiunga na kanisa, kushawishiwa waende kwenye dansi ama kitu fulani. Wanajaribu kuridhisha kitu hicho kitakatifu ambacho Mungu aliweka ndani yao kumwonea Yeye kiu. Basi yale wanayofanya, wanajaribu ku—kumwacha ibilisi awaridhishe, kwa kuwapa kitu kingine ambacho hakiridhishi.

Ee Mungu, jalia kiondolewe asubuhi ya leo.

295 Loo, jinsi ningetaka kuliona kundi hili la watu limepakwa mafuta sana na Roho Mtakatifu! Hata mkitoka hapa nje... Kungekuwa tu na kitu kitakachowapata, kitu tu ambacho kingetuondoa sisi sote hapa, mimi pamoja nawe, ewe rafiki, sisi sote pamoja, tutoke hapa chini ya ushawishi wa Roho Mtakatifu, tukawalete watu kwa Yesu Kristo.

296 Sasa huku...kumekuwa na yapata mikono thelathini iliyoinuliwa, wanaotaka kuja, kujiweka sawa na Mungu. Kumekuwa na angalau wanane ama kumi, ama zaidi ya hao, ambao ni wenye dhambi, ambao hawajawahi kumpokea Yeye.

297 Na tuombe, na chini moyoni mwako uamini. Hivyo tu ndivyo unavyoweza kufanya, ni kuamini. Ni juu ya Mungu kufanya yaliyosalia. "Ibrahimu alimwamini Mungu, na akahesabiwa kwamba ana haki." Hayo ndiyo yote Ibrahimu aliyoweza kufanya. Ilimbidi kuamini. Ikambidi Mungu kufanya hesabu. Hivyo tu ndivyo unavyoweza kufanya ni kuamini. Kwa uaminifu tu sasa inamisha kichwa chako juu ya meza yako ama popote ulipo, na hebu tuombe.

298 Bwana Mungu, ninatambua, kama kulikuwako na mkono mmoja tu, ni maombi ya jinsi gani ningaliomba kwa ajili ya mtu huyo? Jinsi tu Roho Mtakatifu angeuongoza moyo wangu.

299 Wakati mmoja niliketi mahali walipo, kama mwenye dhambi, pasipo kumjua Kristo na wokovu Wake. Siku moja nikakukubali Wewe, Bwana. Sikujua jinsi ya ku. . . [Sehemu ttupu kwenye kanda—Mh.] Kamwe sitasahau hilo. Bwana, liliyabadilisha maisha yangu. Na mimi ninajua hilo si kinyume na Neno. Liko pamoja na Neno.

300 Kwa hiyo, Baba, kwa njia yangu nyenyekevu ya kufanya jambo hilo, je, utawapokea hao walioinua mikono yao? Na hata wale ambao hawakuinua, endapo wana haja, wapokee, Bwana.

301 Ondoa ulimwengu wote. Ondoa tamaa zote za ulimwengu. Ziondoe kutoka kwa ndugu zangu, kutoka kwa dada zangu. Ziondoe kutoka kwangu, Bwana. Mimi niko pamoja nao. Sote tuko katika hekalu la Mungu. Nasi tunatambua ya kwamba, udogo wetu, jinsi tulivyo wadogo, Bwana, jinsi tulivyo wadogo na wasio na maana, na jinsi Wewe ulivyo mkuu.

302 Ee Yehova, warehemu hawa wenye dhambi. Ninasihi kwa ajili yetu sote, Bwana. Lichukue kundi hili dogo pamoja na mimi, asubuhi ya leo. Tusafishe, Bwana. Tufanye viumbe vipya. Sivyo, tafadhali? Katika maskini njia yangu nyenyekevu ya kukuomba Wewe, Baba, ninatoa hili katika Jina la Yesu Kristo, kwamba Wewe utawapokea.

303 Sasa ninajikabidhi mwenyewe kwa Mungu. Ninazikabidhi njia zangu, mawazo yangu yote, matendo yangu. Jalia nisiwaze tena mawazo yangu. Jalia nisiwe tena na njia zozote za ulimwengu. Zote na zitakaswe. Jalia niwe tu na mawazo safi, matakatifu, tangu leo na kuendelea. Jalia maisha yangu yote yawe Yake.

304 Nena kupitia kwangu. Na, Bwana, ni—nisingesema, ufanye hivyo, isipokuwa Wewe umelikusudia. Uliikusudia Injili Yako ihubiriwe na wanadamu. Ungeweza kuukusudia upepo kuihubiri. Ungeweza kuzikusudia nyota kuihubiri. Ungeweza kuukusudia mwezi, jua, kuihubiri. Ila uliwakusudia wanadamu. Yeye hatalibadilisha. Unawangojea wanadamu. Huzingojei nyota; hizo zinakutii. Upepo utakutii. Bali, Bwana, sisi wanadamu, hatufai kitu, hatukutii. Bwana, tusamehe, sivyo? Hivi hutatusamehe?

305 Tusamehe, Bwana, na utufanye wahudumu, sisi sote, kila mmoja katika njia yake—yake mwenyewe, kila mmoja katika mazingira ya—yake mwenyewe, kila mmoja katika njia yake mwenyewe, ambapo anaweza kufanya vizuri zaidi. Tunajikabidhi tu Kwako sasa. Tufanye watumishi Wako, wahudumu wa Neno. Katika Jina la Yesu ninaomba dua hili.

306 Nawe ulitufundisha sote kwamba inatupasa kuomba hivi:

Baba yetu, uliye mbinguni, Jina Lako Litukuzwe.
Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yafanyike hapa duniani kama ilivyo Mbinguni.
Utupe leo riziki yetu.
Na utusamehe dhambi zetu, kama sisi nasi tunavyowasamehe wale watukoseao.
Usitutie katika majaribu, bali utuokoe na uovu; kwa kuwa ufalme ni Wako, nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.

307 Kamwe usiliache life. Amina.

Anakujali,
Anakujali,
Kupitia mwangaza wa jua ama kivuli,
Anakujali.

308 Hivi Yeye hakulielezea? Sasa, moja kwa moja mezani, hebu tupeane mikono. Endeleeni tu kuketi.

Anakujali . . .

Useme, "Mungu akubariki, msafiri."

Anakujali,
Kupitia . . .

63-0112 Ushawishi
Ramada Inn
Phoenix, Arizona Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org